SUPA JACKPOT
TZS. 1,093,395,265
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Watalii** waanza kuondoka Kenya, Odinga adai kutishiwa kuuawa

UKURASA 3


ama
AFYA NA MAZINGIRA
Vita ndoa za utotoni ilivyochachamaa
Ilivyo vita vya kukabili kasi HIV, dawa kulevya Mwanza
ZAMA AWAMU YA SITA...
**Ofisi Makamu Rais yaanika hatua zake katika mazingira**
• Safari imeanza mkakati 2022-32

UKURASA 11

Nipashe
Alhamisi Machi 23, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581258
www.ippmedia.com
The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# TEC yashauri kinga viongozi kutokushtakiwa iondolewe

UKURASA 2


## YALIYOMO

UKURASA WA 4
**OLENGURUMWA ATAKA WAPINZANI KUMWACHIA SAMIA URAIS 2025**
MRATIBU wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Olengurumwa, ameshauri wapinzani...

UKURASA WA 4
**NCHEMBA APIGIA DEBE UINGEREZA KUONGEZA MIRADI UWEKEZAJI**
TANZANIA imelishauri Shirika la Kimataifa la Uwekezaji la Uingereza (BII) kuongeza kiwango cha uwekezaji...

UKURASA WA 7
**NEMC YATOA DARASA UTOKOMEZAJI MIFUKO**
BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limeshiriki maonyesho ya Kimataifa ya Kilimo na Mazingira...


Jaji Mkuu mstaafu, Mohamed Chande Othman



"Mapendekezo yetu ni kuona mahakama ikitoa haki kwa uhuru bila kuingiliwa na chombo chochote itoe haki kwa usawa.

**Askofu Kisare**



"Katiba inatamka kwamba watu wote ni sawa mbele ya sheria na wakati huo huo inaweka kinga ya kutoshtakiwa kwa baadhi ya viongozi.

**Dk. Kassala**

## WHO yatuma timu kuchunguza ugonjwa Marburg

UKURASA 3



## Kipindupindu chaua watatu, 72 waugua

UKURASA 2

MICHEZO **REKODI UGANDA VS STARS ZASHTUA** UK.24
**KATUNI** UK.6




Shekhe Mkuu wa Tanzania, Mufti Abubakari Zuberi (wa tatu kulia), akikabidhi msaada wa vyakula mbalimbali vya futari kwa ajili ya maandalizi ya mwezi Mtukufu wa Ramadhan kwa mtu mmoja kati ya 200 jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mwenyekiti Khidmatul Ummah, Arif Surya. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# TEC yashauri kinga viongozi kutoshtakiwa iondolewe

**Na Restuta James**

BARAZA la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), limetaka watu wote kuwa sawa mbele ya sheria na kutaka mfumo wa hakijinai usiweke kinga ya kutoshtakiwa kwa baadhi ya viongozi umma.

Aidha, Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), limetaka sheria ya ndoa inayoruhusu mtoto wa kike kuolewa akiwa na miaka 14 ibakie kama ilivyo.

Viongozi hao wa dini walitoa maoni hayo Dar es Salaam jana mbele ya Tume ya Kurekebisha Mfumo wa Haki Jinai, inayoongozwa na Jaji Mkuu Mstaafu, Othman Chande.

Mkurugenzi wa Hadhi ya Utu wa Mwanadamu kutoka TEC, Dk. Camilius Kassala, alisema Katiba inatamka kwamba watu wote ni sawa mbele ya sheria na wakati huo huo inaweka kinga ya kutoshtakiwa kwa baadhi ya viongozi.

Baadhi ya viongozi wenye kinga ya kutoshtakiwa ni Rais, Spika wa Bunge, mwendesha mashtaka wa serikali na majaji.

Alisema kinga ya kutoshtakiwa kwa baadhi ya watu ni kinyume cha utu kwa kuwa watu wote wako sawa mbele za Mungu bila kujali hadhi yao kidunia.

"Kuweka kinga ya kutoshtakiwa ni makosa ndiyo maana kuna vuguvugu la Katiba Mpya ili hiyo kinga iondolewe. Watu wameanza kuelewa kwamba sisi binadamu wote tuko sawa kama alivyotufundisha Baba wa Taifa Mwalimu (Julius) Nyerere. Uwe Rais usiwe Rais sote tuko sawa.

"Mwanadamu ni sura na mfano wa Mungu ana hadi yake. Awe gerezani kama mfungwa, mtuhumiwa, tajiri, bosi, kamanda wa polisi au rais...hadhi ya kila binadamu ni sawa," alisema.

Alipendekeza kuwa mfumo wa hakijinai utoe mamlaka kwa wananchi kuishtaki serikali pale wanapoona haijatimiza wajibu wake ipasavyo hususani inaposhindwa kusimamia haki za raia.

Dk. Kassala alifafanua kwamba watendaji katika vyombo vya hakijinai kuanzia polisi, mahakama, magereza na mawakili, wanapaswa kuzingatia utu pale mtuhumiwa anapokamatwa hadi anapohukumiwa.

Kuhusu mahakama, alipendekeza kuwa mfumo uboreshwe ili uzito wa adhabu uendane na hadhi ya mahakama pamoja na uhalisia wa mtuhumiwa.

Alitoa mfano kwamba Mahakama za Mwanzo zinashughulikia makosa madogo pamoja na wananchi wa kipato cha chini, hivyo iwekewe ukomo wa faini kwani mara nyingi zinakuwa kubwa jambo linalotoa mwanya wa rushwa.

Kwa upande wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), imependekeza utu na haki vizingatiwe kwenye ngazi zote za haki jinai kuanzia polisi, ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP hadi) na mahakamani.

Mkuu wa Kanisa la Mennonite Tanzania, Askofu Nelson Kisare, ambaye amewasilisha maoni ya CCT, alisema watuhumiwa waliopo mahabusu na wafungwa, wanapaswa kuhudumiwa kwa kuzingatia utu na haki zao bila kunyanyaswa.

"Mapendekezo yetu ni kuona mahakama ikitoa haki kwa uhuru bila kuingiliwa na chombo chochote itoe haki kwa usawa," alisema.

Mwanasheria Mkuu wa BAKWATA, Hassan Athman, alisema baraza hilo limependekeza maboresho kwenye maeneo mengi ikiwamo ya mwenendo wa makosa ya jinai, ugaidi, uhujumu uchumi, utakatishaji fedha na kutaka sheria ya ndoa ibakie kama ilivyo.

Alisema imani ya Kiislamu inaruhusu mtoto kuolewa anapovunja ungo, hivyo sheria ya ndoa kutoa ruhusa ya mtoto kuolewa kwa ruhusa ya mahakama ni jambo wanaloliunga mkono.

"Kuna ukinzani katika sheria ya ndoa, sheria ya mtoto na katika imani...sisi Waislam tunaamini kijana wa kiume anapobalehe anaruhusiwa kuoa na binti anaruhusiwa kuolewa anapovunja ungo. Haijalishi kavunja ungo akiwa ana miaka 10, 12, 13. Kiimani sisi tunaruhusiwa," alisema.

"Tumependekeza kwamba kifungu kinachoruhusu umri wa miaka 14 kibaki mtu aruhusiwe kuolewa," alisema.

Pia alipendekeza sharti la dhamana ya mtumishi wa serikali kwa mtuhumiwa liondolewe, kwa kuwa wapo raia wengi waadilifu wanaweza kuwadhamini ndugu zao pale watakapokabiliwa na kesi.

Alisema BAKWATA pia imependekeza kwamba mfumo urekebishwe ili DDP asifungue kesi ya jinai mahakamani kama hajakamilisha upelelezi.

## Kipindupindu chaua watatu, 72 waugua

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema katika kipindi cha Februari hadi Machi, 2023, watu 72 wameugua ugonjwa wa kipindupindu na wengine watatu wamefariki dunia katika mikoa minne, huku ikizindua mpango shirikishi wa taifa wa kuzuia na kukabili.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, aliyasema hayo jana alipokuwa akizindua mpango huo jijini hapo.

Simbachawene alisema ugonjwa huo uligundulika Februari 19, hadi Machi 15, 2023, wamepokea taarifa ya wagonjwa 60 ambao kwa Mkoa wa Ruvuma ni 13, Kigoma (7), Katavi (34) na Rukwa (18).

"Tanzania ilishuhudia kipindi kirefu cha mlipuko wa kipindupindu hapa nchini kuanzia mwaka 2015 hadi 2018. Mlipuko huo ulitupa uzoefu mkubwa katika kukabiliana na ugonjwa huo hatari.

Hata hivyo, mlipuko wa ugonjwa huu umepungua katika sehemu kubwa ya nchi yetu," alisema.

Akizungumzia mpango huo, Simbachawene alisema ulifanyiwa mapitio na utaiwezesha serikali kuimarisha shughuli za uratibu na kuweka mifumo madhubuti ya kisekta ya kukabiliana na ugonjwa huo hatari.

"Huu mpango utaziwezesha wizara zinazohusika, Idara, Taasisi, Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa kushiriki kikamilifu katika hatua za kuzuia, kujiandaa kukabiliana na ugonjwa wa kipindupindu na kurejesha hali pindi ugonjwa huo unapotokea," alisema.

Hata hivyo, alisema katika tathmini iliyofanyika ya ugonjwa huo ilitaja sababu za kujirudia kwa milipuko kwenye maeneo mbalimbali unaotokana na ukosefu wa majisafi na salama kwa jamii husika, uelewa mdogo wa namna ya kujikinga na kupambana na ugonjwa huo na jamii kukosa vyoo bora na matumizi hafifu ya vyoo. Kadhalika, alisema taarifa kutoka Shirika la Afya Dunia (WHO) inaeleza kuwapo na mlipuko mkubwa wa kipindupindu nchini Malawi na hadi kufikia Machi 15, 2023 kulikuwa na jumla ya wagonjwa 53,925 na vifo 1,658 vilivyotolewa taarifa.

"Taarifa hii inatupa tahadhari ya mlipuko huo pia kuvuka mipaka na kuingia nchini kwetu hususani pale tusipo imarisha afua mbalimbali za kujikinga na kipindupindu kwa jamii zetu hususani kwa mikoa inayopakana na nchi hiyo, tetesi za kuwapo kwa mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu pia zipo kwa nchi nyingine tulizopakana nazo kama Msumbiji, DRC Congo, Zambia na Kenya," alisema.

Aliihimiza Wizara ya Afya kuongeza nguvu ya ufuatiliaji ili kuhakikisha wagonjwa na tetesi zote zinatolewa taarifa na kutibiwa mapema kwenye vituo vya kutolea huduma kabla ugonjwa haujsambaa kwenye maeneo makubwa zaidi.

"Naelekeza Ofisi za tawala za Mikoa na Halmashauri zote kushirikiana na mamlaka za maji mijini na vijijini (RUWASA), ili kuhakikisha hali ya upatikanaji wa maji katika maeneo yao inaimarika," alisema.

# WHO yatuma timu kuchunguza ugonjwa wa Marburg

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limetuma timu ya dharura mkoani Kagera kufanya uchunguzi zaidi wa mlipuko wa ugonjwa wa Virusi vya Marburg (MVD), ulioripotiwa na kuua watu watano mpaka sasa.

Mkurugenzi wa WHO Kanda ya Afrika, Dk. Matshidiso Moeti, alisema juhudi za mamlaka za afya za Tanzania kubaini chanzo cha ugonjwa huo ni kielelezo tosha cha dhamira ya dhati ya ukabiliana nao.

Kupitia taarifa iliyotolewa juzi na Shirika hilo, Dk. Moeti alisema wanafanya kazi kwa pamoja na serikali kuongeza kasi ya udhibiti na kukomesha kuenea kwa virusi hivyo haraka iwezekanavyo.

Dk. Moeti alisema timu ya dharura ya WHO itaangazia kutafuta visa katika jamii na vituo vya afya mkoani humo, ili kubaini mwingiliano zaidi na kutoa huduma zinazohitajika.

"Tutaendelea kufanya kazi kwa karibu na mamlaka ya afya ya kitaifa kuokoa maisha," alisema.

Juzi, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu alithibitisha kutokea kwa mlipuko wa ugonjwa huo wilayani Bukoba mkoani Kagera, ikiwa ni siku nne baada ya kuwapo kwa taarifa za watu watano kufariki dunia akiwamo mhudumu wa afya ambaye alipata dalili za ugonjwa huo na wanane wakiripotiwa kuugua.

Alisema mpaka sasa serikali imefanikiwa kuudhibiti, ili usienee maeneo mengine na inaendelea kuwafuatilia watu 161 wanaohisiwa kuchangamana na wagonjwa hao.

"Uchunguzi tuliofanya katika maabara yetu, umethibitika kuwapo kwa virusi Marburg, uliogundulika mwaka 1967 huko Ujerumani, mji wa Marburg ndio asili ya jina hili," alisema.



Wachuuzi wa mboga na matunda wakiwa wamepanga bidhaa zao juu ya mfereji wa maji ya mvua kando ya barabara ya Morogoro, eneo la Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam hivi karibuni, wakidai kukosa maeneo ya kufanyia biashara. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Watalii waanza kuondoka Kenya, Odinga adai kutishiwa kuuawa

**Na Maulid Mmbaga**

MBALI na hasara ya Sh. bilioni mbili inayotajwa kupotea kutokana na maandamano yaliyofanyika nchini Kenya mwanzoni mwa wiki hii, inaelezwa kuwa sekta ya utalii imeathirika zaidi kutokana na watalii wengi kuanza kuondoka wakihofia usalama wao.

Jana katika mitandao ya kijamii kilirushwa kipande cha video kinachoonyesha msururu wa raia wa kigeni wakiwa wamebeba mabegi wakiingia katika Uwanja wa Ndege wa Jomo Kenyatta, wakifanya jitihada za kutaka kuondoka nchini Kenya wakihofia machafuko yaliyosababishwa na wafuasi wa kiongozi wa upinzani Raila Odinga wakati wa maandamano.

Imeelezwa kuwa hali hiyo itasababisha hasara kubwa katika hoteli za kitalii, sekta ya utalii na taifa la Kenya kwa ujumla, na pamoja na matokeo hayo, kiongozi mkuu wa upinzani nchini Kenya Raila Odinga ametoa wito kwa wafuasi wake kufanya maandamano mara mbili kwa wiki hadi serikali itakapofanyia kazi madai yao.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya ndani, Jumatatu wiki hii Odinga aliitisha maandamano yanayotajwa kusababisha ghasia katika maeneo mbalimbali nchini humo hasa jiji kuu la Nairobi na Kisumu, huku polisi wakisema mwanafunzi mmoja aliuawa na wengine 200 kukamatwa.

Sababu ya Odinga kuitisha maandamano hayo ni kuipinga Serikali ya Rais William Ruto kuhusu kupanda kwa gharama za maisha.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kamanda Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini Kenya, Japheth Koome, baadhi ya waandamanaji waliwasha moto mitaani na kuwarushia mawe polisi.

Alisema Polisi walifyatua mabomu ya kutoa machozi na kuwarushia maji yanayowasha waandamanaji hao ukiwamo msafara wa Odinga aliyekuwa akiwahutubia wafuasi wake kutoka kwenye paa la gari yake.

Pia, alisema maofisa 24 walijeruhiwa katika mapambano hayo, lakini hawakutoa idadi ya waandamanaji waliojeruhiwa.

"Mapambano hayo ya siku nzima yaliyoshuhudiwa huko Nairobi na Kisumu hayakuwa na msingi zaidi ya kufanya ghasia dhidi ya polisi na kuhujumu uchumi," alisema.

**MADAI YA KUUAWA**

Hata hivyo, Kiongozi wa Azimio Odinga, alidai kuwa kulikuwa na jaribio la maofisa wa usalama kumwangamiza yeye pamoja na Kalonzo Musyoka wakati wa maandamano ya Jumatatu.

Alisema maofisa wa usalama waliwafyatulia magari yao risasi wakati wa maandamano jijini Nairobi jambo ambalo liliwashtua.

"Kulikuwa na jaribio la kuangamiza Raila Odinga na Kalonzo Musyoka. Magari yao yalilengwa na risasi, lakini kwa bahati mzuri hawakupata majeraha. Tunaendelea kushangazwa na kitendo hicho cha polisi," alisema Odinga.

**ODINGA AKAMATWE**

Kutokana na ghasia hizo, wabunge wa chama tawala UDA waliitaka serikali kumchukulia hatua na kumkamata kinara wa Azimio Odinga kwa madai kuwa maandamano aliyoyaitisha yalisababisha uharibifu wa mali za Wakenya.

Wabunge hao walitoa taarifa kwa wanahabari wakiongozwa na Gavana Cecil Mbarire, wakisema kuwa Odinga, aliongoza maandamano yaliyoleta vurugu sehemu kadhaa katika taifa hilo.

"Jumatatu Raila aliongoza kundi lake la waporaji kutatiza amani na utulivu wa Jiji la Nairobi na sehemu kadhaa nchini. Odinga aliongoza vurugu iliyosababisha kuharibiwa kwa mali na kutatizika kwa biashara nchini," alisema Mbarire.

Wabunge hao wa UDA pia walitoa wito kwa vitengo vya usalama kuanzisha mchakato wa kumshtaki Odinga na viongozi wengine wa mrengo wa Azimio kwa uharibifu wa mali na maisha yoyote yaliyopotezwa wakati wa maandamano.

"Wao kama Azimio wanastahili kushtakiwa kwa uharibifu na uporaji wa mali na pia kwa maafa yoyote yaliyompata mtu wakati wa maandamano," alisema Mbarire.

Vile vile, Mbarire aliwapongeza maofisa wa usalama ambao anasema walifanya kazi nzuri iliyohakikisha kuwa utulivu unarejea licha ya purukushani iliyoshuhudiwa.

**VIONGOZI WA DINI**

Baadhi ya viongozi wa Kiislamu wametoa wito kwa Odinga kusitisha maandamano wakati wa ibada ya mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhani

Katibu wa Muungano wa Maimamu nchini humo, Shekhe Mohamed Khalifa, alisema wanatarajia kuanza kufunga kwa maombi ya mwezi wa Ramadhani kuanzia leo, Machi 23.

Katibu huyo alimtaka Raila kuwaheshimu waislamu watakaokuwa wanafunga kwa maombi kwa kusitisha maandamano aliyoyaitisha.

"Wakati wa mwezi mtukufu wa Ramadhani Mwenyezi Mungu huweka kando mashetani yote ili kumpa muislamu wakati mwafaka wa kuswali, waheshimu waislamu kwamba ni mwezi wao wa ibada, tunawasihi wale wote wanaohusika katika mipango hii ya maandamano kuuheshimu mwezi huu mtukufu wa Ramadhani na pia kuwaheshimu waislamu," alisisitiza Khalifa.

Shekhe Mohammed Dor, miongoni mwa viongozi wa kiislamu, alisema kuwa ipo haja ya makubaliano na maelewano ya haraka kuhusu mzozo unaoshuhudiwa.

"Kuna haja ya kutafuta mbinu mwafaka itakayoweza kusuluhisha mzozo unaoendelea na kuwapa fursa Wakenya muda mwafaka wa kubuni njia za kujenga uchumi wa taifa," alisema Dor.

Aidha, viongozi wengine wa madhehebu mbalimbali wamejitokeza na kuomba kuwe na makubaliano kati ya makundi mawili ya kisiasa yanayozozana kwa manufaa ya maendeleo ya taifa hilo.

Katibu Mkuu wa chama tawala (UDA), Cleophas Malala, alidokeza kuwa kuna uwezekano wa maridhiano kati ya Rais Ruto na mpinzani wake Odinga.

# Olengurumwa ataka wapinzani kumwachia Samia urais 2025

**Na Christina Mwakangale**

MRATIBU wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Olengurumwa, ameshauri wapinzani kutosimamisha wagombea urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Amesema kwa mtazamo wake, kutokana na Rais Samia Suluhu Hassan kuonyesha nia ya majadiliano na upinzani, huku vyama vya siasa vikianza kurejea tangu kufungiwa shughuli zao kwa takribani miaka saba, ni vyema vikaacha nafasi hiyo ili kukuza utawala bora.

Olengurumwa aliyasema hayo hivi karibuni kwenye mahojiano akizungumzia miaka miwili ya Rais Samia madarakani huku akisisitiza kuwa hiyo ni hoja yake binafsi.

"Kwa mimi nataka niwashauri vyama vilivyoshindwa kufanya kazi. Tanzania tuliua upinzani, hivyo kwanza wajipange. Upinzani wawekeze kwa ajili ya uchaguzi unaokuja wa serikali za mitaa na kwa uchaguzi wa mwaka 2025 wawekeze kwenye madiwani na ubunge.

"Wafanye hivyo hivyo angalau wapate wapate theluthi ya wabunge, theluthi madiwani na wenyeviti wa vijiji. Wakifanya hivyo kwa uchaguzi unaokuja wa mwakani (serikali za mitaa) na uchaguzi mkuu mwaka 2025, hadi uchaguzi wa mwaka 2030 wataweza kusimamisha wagombea urais. Uchagzui wa 2025 ukiwa wa haki wapinzani watapata viti vya ubunge, udiwani na mitaa. Waingie makubaliano na rais katika uchaguzi huru na haki," alisema.

Alisisitiza kuwa ili kuwa na mgombea urais ni pesa, na kwa uhalisia wapinzani pia wana tatizo hilo, hivyo wawekeze kwa wagombea udiwani na ubunge. Olengurumwa alisema kwa mtazamo Rais aliyeko madarakani anatekeleza misingi yao (wapinzani) kama vile haki ambayo imetolewa na sasa wanafanya shughuli zao za kisiasa.

"Tumuunge mkono hata kama vyama havitanufaika kisiasa sasa lakini tutakuwa tumeepusha kizazi kwa miaka ijayo kuja kuwa na siasa za chuki," alisema.

Kuhusu mtazamo wa asasi za kiraia (AZAKI) juu ya masuala ya utawala bora nchini, alisema ukimya wa matamko unamaanisha uwapo wa kiwango cha haki za binadamu, usawa na uhuru wa vyombo vya habari.

"Rais Samia Suluhu Hassan kwa kipindi cha miaka miwili tangu aingie madarakani na kuigusa katiba hasa kwenye eneo la utawala bora na haki, sasa mifumo hiyo ilindwe kitaasisi na kisheria. Tutaonekana ni watu ambao hatujui tunachokitaka, kusimama na kuanza kupinga hakuna sababu, amerudisha demokrasia, ameshiriki mikutano na wapinzani.

"Kimsingi watetezi wa haki za binadamu tunataka tuone viongozi wetu wakiheshimu haki za binadamu, kiongozi akiwa kinyume na utawala bora utatuona sisi tukiwa mbele na matamko ya kushauri," alisema.

Hata hivyo, alisisitiza kuwa kuna haja ya kuwa na bunge bora ambalo linaweza kukosoa na kutoa mwelekeo ambao una dhamira njema kwa taifa.

"Tulifika hatua bunge lilikuwa na wabunge karibu nusu kwa nusu, mabadiliko tunayoyaona yalitokana na bunge. Kama Escrow ilitokana na mijadala ya wabunge wa pande zote," alisema.

Pia alisema mihimili mingine pia ambayo inahitaji kuimarishwa na kiongozi wa nchi na kuwa na uhuru kwenye utendaji wao ni mahakama na vyombo vya habari ambavyo hutoa mchango mkubwa wa kuibua kero, yakiwamo masuala ya rushwa.

Ole Ngurumwa, alieleza kwamba utashi wa kisiasa aliouonesha Rais Samia, ni mwanzo wa ujenzi mpya wa siasa za kistaarabu na za kuigwa barani Afrika.



Meya wa Manispaa ya Kinondoni, Songoro Mnyonge, akipanda mti wakati akizindua kampeni ya utunzaji wa mazingira katika Wilaya ya Kinondoni eneo la Kwa Mtogole, Dar es Salaam jana, kampeni hiyo inasimamiwa na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) na Bodi ya Bonde la Wami Ruvu ofisi ya Dar es Salaam. **PICHA: FRANK MONYO**

# Nchemba apigia debe Uingereza kuongeza miradi uwekezaji nchini

**Na Benny Mwaipaja,** LONDON

TANZANIA imelishauri Shirika la Kimataifa la Uwekezaji la Uingereza (BII) kuongeza kiwango cha uwekezaji nchini ili kukuza biashara. Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alitoa wito huo jana jijini hapa alipoongoza ujumbe wa Tanzania uliokutana na menejimenti ya shirika hilo, ambalo limewekeza katika baadhi ya miradi nchini. Alisema Tanzania ina fursa nyingi za uwekezaji katika sekta mbalimbali zikiwamo nishati, kilimo, utalii, madini, viwanda na huduma na rasilimali za asili kama vile gesi na maji kwa ajili ya kuzalishaji wa nishati. Dk. Nchemba alizitaja rasilimali zingine kuwa ni ardhi yenye rutuba kwa ajili ya kilimo, madini na hali ya amani nchini, ambavyo kiujumla vinaweka mazingira ya kuvutia kiuwekezaji.

Waziri Nchemba aliialika timu ya wataalamu kutoka BII kutembelee Tanzania na kufanya mazungumzo na taasisi na mashirika mbalimbali pamoja na sekta binafsi ili kuangalia maeneo ya kuwekeza kwa faida ya pande zote zinazohusika.

Naye Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Juma Malik Akil, alisema Zanzibar ikiwa sehemu ya Tanzania, inatekeleza programu ya uchumi wa bluu inayohitaji uungwaji mkono wa taasisi za fedha za kimataifa na kuiomba taasisi hiyo kushiriki katika ujenzi wa uchumi wa Zanzibar.

Mkurugenzi Mtendaji wa BII, Chris Chijiutomi, alihakikishia Tanzania kwamba iko tayari kuongeza uwekezaji kwa kushirikiana na sekta binafsi ikiwa ni sera ya serikali ya Uingereza na misingi ya kuanzishwa kwa shirika hilo.

Alisema shirika lake lina mtaji wa zaidi ya dola za kimarekani bilioni 11 lakini imewekeza Tanzania Dola milioni 215 pekee, hivyo kuitaka Tanzania kuainisha miradi ya kipaumbele ambayo shirika hilo litachambua na kutoa fedha kwa kushirikiana na sekta binafsi.

# WaterAid yaweka mkakati kumaliza kero maji

**Na Beatrice Shayo**

SHIRIKA la WaterAid Tanzania linatarajia kuzindua mpango mkakati wenye matarajio makubwa wa miaka mitano Mei, mwaka huu, utakaomaliza tatizo la maji na usafi wa mazingira.

Akizungumza wakati wa maadhimisho ya Siku ya Maji Duniani nchini Tanzania, Mkurugenzi Mkaazi wa Shirika la WaterAid, Anna Mzinga, alisema mkakati huo utaanza mwaka huu hadi 2028 kuhakikisha kila mtu wanapata huduma ya majisafi na salama ambayo pia ni endelevu.

Mzinga alisema wataendelea kushirikiana na washirika kuunga mkono na kushawishi sera na bajeti, ili kuchangia katika kuboresha upatikanaji wa huduma salama, nafuu, zinazozingatia jinsia, jumuishi kijamii na endelevu, huduma za majitaka na usafi kwa kila mtu na kila mahali.

"Tunajua kwamba upatikanaji unaotegemewa wa maji na usafi wa mazingira unaosimamiwa kwa usalama pamoja na desturi na rasilimali za usafi wa kiafya, huwawezesha watoto, familia na jamii kuwa msingi wa kudumu wa kuboresha afya, uchumi imara na fursa kubwa zaidi," alisema.

Alisema huduma za maji na usafi wa mazingira zinahitaji kuendelezwa kwa kiasi kikubwa, ili kufikia maendeleo yanayohitajika katika afya na ustawi ambayo yatasaidia nchi kujenga uwezo wa kustahimili siku zijazo na kutimiza uwezo wake.

"Tunatamani kuwa mahali ambapo hakuna jamii inayorudishwa nyuma na magonjwa yasiyo kwisha yanaosababishwa na miundombinu mibovu ya majitaka, afya na usafi wa mazingira. Hakuna msichana anayepaswa kutengwa na maisha bora ya baadaye kwa sababu shule yake haina vyoo vinavyofanya kazi vilivyo na milango ya kufunga au chumba cha usafi wa hedhi," alisema Mzinga.

Alisema hakuna mtu anayepaswa kuachwa nyuma kwasababu ya ukosefu wa maji Siku ya Maji Duniani ni siku inayotambuliwa na Umoja wa Mataifa ambayo inataka kuunga mkono kufikiwa kwa lengo la sita la Maendeleo Endelevu kuwa maji na usafi wa mazingira kwa wote ifikapo mwaka 2030.

Pia alisema mwaka huu wanapotumia kaulimbiu ambayo inasema "Kuhakikisha Upatikanaji wa Maji Katika Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi," ni fursa nzuri kwa WaterAid kusisitiza umuhimu wa usimamizi na uendelevu wa rasilimali za thamani za maji na kuwasisitiza watoa maamuzi kuchukua hatua katika kukabiliana na tatizo la maji duniani.

"Kwa wasichana, upatikanaji wa vifaa vya WASH ni jambo muhimu linaloathiri mahudhurio ya shule, hasa wakati wa hedhi na ni moja ya sababu kuu za wasichana kuacha shule.

Asilimia 34 ya wasichana waliripotiwa kukosa masomo wakati wa hedhi kutokana na ukosefu wa vyumba vya kubadilishia nguo na asilimia 26 walilaumu ukosefu wa choo safi na kinachofaa," alisema.



Baadhi ya wafanyakazi wa Kampuni ya bia ya Serengeti (SBL) Mwanza, na wa Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria, wakifanya usafi kwenye Mto Mirongo jijini Mwanza jana, kama sehemu ya kuadhimisha Siku ya Maji Duniani. Mto Mirongo hupeleka maji yake kwenye Ziwa Victoria. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC apiga marufuku uvunaji miti ya asili

**Na Mwandishi Wetu,** KIGOMA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Dk. Batilda Buriani, amepiga marufuku uvunaji na usafirishaji wa nguzo za miti kwenye misitu ya asili mkoani humo inayopelekwa kwenye shughuli za madini Kanda ya Ziwa na ukaushaji wa tumbaku.

Dk. Buriani alitoa maagizo hayo karibuni kwa Kitengo cha Misitu na kuwataka kuacha moja ya utoaji vibali vya ukataji na usafirishaji wa bidhaa hizo za misitu, ambavyo vinatoa ruhusa kwa wafanyabiashara, wakulima na wajasiriamali kufanya shughuli hiyo.

Alitoa maagizo hayo akiwa kwenye ziara ya mafunzo iliyoandaliwa na Kampuni ya Tumbaku ya Alliance One katika wilaya za Uvinza, Buhigwe na Kasulu mkoani Kigoma, ambako inatekeleza mradi shirikishi wa upandaji miti katika zaidi ya ekari 1,412 kuanzia mwaka 2014 hadi mwaka jana.

Kampuni hiyo yenye makao makuu yake mkoani Morogoro, lakini ikiwa na matawi nchini kote kunakolimwa tumbaku, ikiwamo Tabora na Kigoma, inapanga kuanzisha mradi mkubwa wa upandaji miti mkoani Tabora, ambako ndiko kwenye ngome yake ya zao la tumbaku, kwani mkoa huo unazalisha ziaidi ya asilimia 60 ya zao hilo nchini.

"Kampuni iliponialika kuja hapa Kigoma kuangalia mradi wao huu, kabla hawajauanzisha kule Nzega, mimi nilifikiri ndiyo kwanza miti ni midogo, kumbe hali ni tofauti, mradi umefanikiwa sana, miti imekuwa ni mikubwa na tayari umeshakabidhiwa kwa wenyewe na watu wameanza kufaidika nao kwa kweli nimefurahishwa sana," alisema.

Mkuu huyo wa mkoa aliikaribisha kampuni hiyo kuwekeza mradi kama huo wilayani Nzega ili kusaidia kuendeleza harakati za upandaji miti, ili kubadili mwonekano wa mkoa huo.

"Ninyi tuelezeni tu ukubwa wa ardhi mnayoitaka, na sisi tutakaa na watu wetu katika kila wilaya na kuwapeni ardhi hiyo haraka, ili upandaji wa miti hii ukatusaidie kulinda miti yetu ya asili ambayo sasa inavunwa kila uchao," alisema.

Mkurugenzi wa Uzalishaji wa Alliance One, David Mayunga, mradi huo unatekelezwa katika vijiji 18 mkoani humo, iliyopandwa kwenye shule, hospitali, vikundi vya jamii na watu binafsi lengo likiwa kusaidia upatikanaji wa kuni, kuuza na matumizi ya ukaushaji wa tumbaku.

"Awali mradi wetu haukueleweka vizuri katika jamii ya watu wa wilaya hizi, baadhi wakisema kwamba kampuni imekuja kupora ardhi ya wenyeji, lakini kadri muda ulipozidi kwenda tukaanza kueleweka kidogo kidogo na mpaka tulipofika muda wa kukabidhi na kuondoka wengine wakaanza kulalamika kuwa mbona tunaondoka mapema mno," alisema.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Jamii cha Kizito chenye wanachama 49 katika wilaya ya Buhigwe, Alex Ndagirwe, alisema wameanza kufurahia matunda ya mradi huo kifedha, maana wameanza kuuza miti.

# FMCL yatangaza huduma bora za anga

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya huduma za anga za ugavi na usafirishaji nchini, Freight Management Company Ltd (FMCL), imetangaza mpango mpya wa kutoa huduma bora za anga za ugavi na usafirishaji, kama sehemu ya mchango wake katika kukuza uchumi wa taifa.

"Tunataka huduma za anga za ugavi na usafirishaji ziwe kwenye kiwango bora ndani ya nchi na kimataifa," alisema Ofisa Mtendaji Mkuu wa FMCL, Witness Panga wakati wa mahojiano maalumu na waandishi wa habari Dar es Salaam wiki hii.

Akirejea jitihada na marekebisho yaliyofanywa na serikali katika kuchochea uwekezaji wa sekta binafsi, Witness alisema kampuni yake imejipanga vizuri kusaidia mipango ya serikali inayolenga kuboresha utoaji wa huduma kwenye ugavi na usafirishaji na huduma zingine nchini Tanzania.

Alisema huduma za ugavi na usafirishaji kama nguzo muhimu katika kuchechemua ukuaji wa biashara na uwekezaji ambavyo vinakuza uchumi wa taifa na kuleta maendeleo kwa Watanzania.

"Matokeo chanya katika uchumi wetu yatainua na kuboresha hali ya maisha ya Watanzania wa kawaida," alisema Ofisa Mtendaji Mkuu wa FMCL, akiongeza kwamba: "Kwa vile sisi ni sehemu ya jamii hii, mchango wetu kwa maendeleo haya ni muhimu na haukwepeki."

Alisema kampuni yake ina wabia wenye mtandao mkubwa na ulioimarika, unaoiruhusu kampuni kutoa huduma zinazoaminika na zenye gharama nafuu kwa wateja wake (wa ndani na kimataifa).

Kampuni ya FMCL inatoa huduma za anga za ugavi na usafirishaji, ambazo ni pamoja na usafirishaji wa mizigo kwa njia ya anga, usafirishaji wa kuunganisha kwa njia ya anga, kubadili meli/kuhamisha shehena na huduma za kukodisha.

Kampuni inatoa pia huduma za ushauri na uchanganuzi. "Wafanyakazi wetu wana uzoefu wa kuweza kutoa suluhisho lilolo bora zaidi kwa mchororo wa mahitaji ya ugavi na usafirishaji."

Katika kufanya kazi zake, Freight Management inatoa huduma za usafirishaji wa kimataifa kwa njia ya anga na baharini kutoka huduma za usafirishaji wa kawaida hadi changamani.

Kimsingi, FMCL ina uwezo wa kutoa huduma yoyote ya usafirishaji, kutoka vifurushi vidogo hadi makontena makubwa. Wafanyakazi wetu wazoefu wanajituma kuhakikisha shehena za wateja wetu zinafika muda wake, salama na ndani ya bajeti.

"Tunajivunia pia huduma ya usafirishaji wa mizigo baina ya nchi na nchi, tukitoa kwa wateja wetu fursa za uchaguzi wa njia ya kutumia, kwa viwango nafuu zaidi na kwa huduma bora.

Huduma za utaratibu wa ugavi na usafirishaji ni pamoja na utakaso wa ushuru, kufunga mizigo, kuhifadhi mizigo ghalani, usambazaji, usimamizi wa orodha/hesabu ya vitu/bidhaa na usafirishaji.


**MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)**

**UTARATIBU WA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA AJIRA ZA MUDA KWA KAYA ZA WALENGWA**

Miradi ya ajira ya muda kwa walengwa wa TASAF ni utaratibu wa utekelezaji miradi ya jamii yenye kutumia nguvu kazi, inayoshirikisha walengwa kufanya kazi na kulipwa ujira. Miradi hiyo inawezesha jamii kupata rasilmali /miundombinu inayotoa huduma na ujuzi kwa jamii kupitia ushiriki wao katika kutekeleza miradi hiyo.

Washiriki wa kazi zinazotoa ajira ya muda kwa walengwa ni watu wenye uwezo wa kufanya kazi wenye umri wa kati ya miaka 18 hadi 65. Kila kaya ambayo inashiriki katika ajira za muda kwa walengwa inaandikisha watu wawili, ambapo mtu mmoja kutoka kwenye kaya ndiye atashiriki kazi kwa wakati mmoja. Utekelezaji wa miradi ya ajira ya muda huchukua miezi sita ambapo walengwa hufanya kazi kwa siku kumi tu kwa kila mwezi. Kwa siku mlengwa anatakiwa kufanya kazi kwa muda usiozidi masaa manne ili aweze kupata muda wa kufanya shughuli nyingine.

Wazee, watu wenye ulemavu, wakina mama wajawazito na wenye watoto wadogo ambao hawajatimiza miaka miwili hawaruhusiwi kufanya kazi za ajira za muda kwa walengwa. Wasimamizi wanaopanga kazi za walengwa hawatakiwi kuwapangia kazi watu hao na wanapaswa kutoa taarifa kwa wajumbe wa kamati ya usimamizi wa mradi (CMC) na Waratibu ili majina ya watu hao yaondolewe kwenye orodha ya watu walioandikishwa kufanya kazi za ajira ya muda. Kaya yenye watu ambao hawaruhusiwi kufanya kazi za ajira ya muda watapokea ruzuku ya msingi.

Uongozi wa TASAF umetoa waraka kwa Wakurugenzi wa Halmashauri na Maafisa Ufuatiliaji kupitia orodha za watu walioandikishwa kufanya kazi kwenye miradi ya ajira za muda na kuwaondoa wale ambao hawaruhusiwi kufanya kazi kwenye miradi hiyo. Aidha utoaji wa elimu kwa viongozi wa jamii, wasimamizi na walengwa kuhusu taratibu za utekelezaji wa miradi ya ajira za muda kwa kaya za walengwa utaendelea kutolewa katika kipindi chote cha utekelezaji.

**Imetolewa na**

**Kitengo cha Habari na Mawasiliano**
**MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII TASAF**

217333102

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanaochakachua mizani waadhibiwe

**KUMEKUWAPO** na malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu upunjwaji wa vipimo wanaponunua bidhaa mbalimbali.

Tatizo hilo linalochangiwa na uchakachauji wa mizani liko katika bidhaa nyingi ambazo mtumiaji analazimika kutumia kwa kipimo.

Kilio cha kupunjwa kinaanzia kwenye bidhaa aina ya nafaka, kitoweo mpaka kwenye mitungi ya gesi.

Baadhi ya wafanyabiashara hufanya uchakachuaji huo ili waweze kupata faida kubwa katika bidhaa atakayouza.

Jambo hili huwaumiza sana walaji kwa sababu wananunua mahitaji kulingana na bajeti ya watu waliopo kwenye familia, lakini wanajikuta kabla siku ambayo amepanga kununua bidhaa nyingine, ile iliyopo inakuwa imekwisha mapema.

Kadhalika kwa wanaotumia gesi ya kupikia nyumbani. Kwenye familia ya watu wachache mtungi mmoja wa kilo 15 unaweza kutumika zaidi ya miezi mitatu kwa aina ya vyakula vinavyopikwa kila mara. Lakini mtungi wenye ujazo huo huo kwa vyakula hivyo hivyo, unaweza usifike miezi miwili kabla ya kununua mwingine.

Watu wengi wanapokwenda kununua bidhaa huchukua bila kuhakiki uhalisi wa uzito uliopo mpaka wanapofika nyumbani na kutumia ndipo hugundua kuwa walipunjwa.

Katika bidhaa ya kitoweo, watu wengi wanalalamika kupunjwa. Kwa mfano mteja anakwenda kununua kilo moja ya nyama lakini anapofika nyumbani anagundua ni nusu kilo na robo.

Uchakachuaji huu unaumiza sana walaji ikizingatiwa kuwa bidhaa nyingi zimepanda bei kutokana na majanga yaliyotokea duniani na kuathiri nchi nyingi.

Baadhi ya wafanyabiashara wanaamua kuwaibia wateja bila huruma na bila kujua huyo aliyejitoa mpaka kununua kilo ya nyama amehangaika kwa kiasi gani ili aweze kufurahisha familia yake siku hiyo ile kitoweo hicho.

Wananchi wengi wanalalamika kuwa wafanyabiashara hao hawafanyiwi ukaguzi wa mara kwa mara na matokeo yake wanabweteka na kufanya wanavyotaka wao.

Kwenye upimaji kuna mizani ya aina mbili, kuna ile inayotumia mawe maalumu ya vipimo na ya kielektroniki.

Katika mizani inayotumia mawe maalumu, baadhi ya wafanyabiashara hutumia ujanja kwa kupunguza kipimo bila mnunuzi kugundua.

Vile vile, mizani mingi haifanyiwi ukaguzi kuona kama inafanyakazi vizuri hali ambayo pia huchangia watejwa kupunjwa.

Wakala wa Vipimo Nchini (WMA), umekuwa ukiwaonya wafanyabiashara kuipeleka mizani yao kukaguliwa mara kwa mara ili kuepuka kuwapunja wateja na kuondoa malalamiko.

Hata hivyo, suala hilo halitekelezwi ipaswavyo na vile vile, mamlaka husika inapaswa kufanya ukaguzi wa kushtukiza ili watu wanaofanya udanganyifu huo waweze kuchukuliwa hatua.

Mamlaka hiyo hata hivyo, inakiri kugundua tatizo hilo ni kubwa na kwa mujibu wa sheria wanafanyakazi usiku na mchana ili mwananchi apate thamani ya fedha ya bidhaa anayonunua.

Mamlaka hiyo pia imewatahadharisha wauzaji wa nyama kuuza kwa uzito sahihi na wamiliki wa maduka hayo wanatakiwa kuhakiki mizani yao kwa sababu sheria itakapochukua mkondo wake, muuzaji na mmiliki wa biashara wote wataadhibiwa.


Wananchi nao wanatakiwa kuwa makini wanapokwenda kununua bidhaa kwa kuzihakiki kama uzito walionunua bidhaa unalingana na thamani ya pesa waliyoitoa.


Kama watakuwa wanahakiki kwa kutaka kupimiwa kwa mara ya pili bidhaa zao, uchakachuaji utakoma na kila mmoja atapata thamani ya bidhaa yake kwa pesa aliyolipa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge

# Hili bodaboda kubeba wanafunzi 'mshikaki', wazazi tuwe makini

Na Yasmine Protace

**KILA** mahali nchini, suala la usafiri wa bodaboda unatawala kwa kina. Ni uchumi, biashara na mfumo wa maisha.

Kila kitongoji cha nchi haukosekani, huku umma hivi sasa ukiamini ndio una uhakika hasa katika suala la kuwahi safari yako, pia kupenya kirahisi kwa gharama nafuu mahali kugumu kufikika.

Kutokana na usafiri huo, kuonekana ni mkombozi kwa kuwakimbiza abiria haraka maeneo waendako, bodaboda sasa ina watumiaji na wateja wa rika mbalimbali.

Faida nyingine ni kwamba, kumekuwapo vijana wengi wanaojiajiri au wengine kuajiriwa, kwenye aina hiyo ya usafiri wa umma.

Kutokana na kundi hilo la vijana wa mijini na vijijini kuingia katika ama ajira au biashara za umiliki usafiri wa bodaboda kuna faida lukuki kimaisha. Si msamiati mpya tena, kusikia mtu anamiliki mradi wa bodaboda, huku maduka ya kuuza pikipiki yakiagiza kutoka kwa wazalishaji nje, yamesambaa kila kona ya miji mikubwa na midogo.

Ndani ya nadharia 'kizuri hakikosi kasoro', kuna la pili hapo, kwamba sasa linakomaa na madhara yake, kuhusiana na nidhamu ya barabarani, hadi lindi la ajali zinazotawala.

Wanashuhudiwa majeruhi wa ajali za bodaboda, hata kujitwalia umaarufu usioafaa katika hospitali za kila mahali nchini.

Waendeshaji hao wanatajwa, wapo ambao wamekuwa wakizijua sheria za usalama barabarani na wapo wasiozijua sheria za usalama barabarani, japo pia ni waendesha bodaboda. Ajali zao ni katika sura ya watoto mapacha.

Pamoja na kutojua sheria za usalama barabarani, lakini kumekuwapo mafunzo ambayo bodaboda huyapata kupitia polisi wa usalama barabarani.

Kutolewa kwa mafunzo hayo, ni sehemu ya kuwawezesha madereva hao wazijue sheria za barabara pale wanapotumia vyombo hivyo.

Niseme na lingine, kwamba suala la bodaboda kubeba wanafunzi na kuwapeleka shule, nisisitize hilo linatakiwa kuangaliwa kwa umakini, ikiwamo kulinda usalama wa watoto pale wanapovitumia vyombo hivyo.

Tayari ama tumesikia au kuiona ajali zake.

Unakuta bodaboda moja imebeba watoto watatu wadogo inawapeleka shule asubuhi na kuwafuata jioni.

Mwendeshaji wa bodaboda hiyo, kwanza hana kofia ngumu, pia kavaa kandambili na anaendesha kifaa hicho, akiwa katika mwendo mkali wa kutisha.

Pindi bodaboda huyo, anapopata ajali amebeba watoto, uzoefu unaoponyesha ni pale anakimbiza usafiri huo, au wakati mwingine anajaribu kulipita gari ili awawaishe wanafunzi shule au nyumbani.

Waendesha bodaboda wengi wanakosa umakini wakiwa barabarani na wakati mwingine, wanawapita, hata kama taa hazijamruhusu, huku akiwa kwenye mwendo mkali na wanafunzi wake.

Tunajua gharama za kulipia usafiri wa shule ni hata baadhi ya familia hazimudu na kuamua kuzama katika mbadala wa majirani kuchangishana fedha, wakiamua kutafuta bodaboda moja itakayowabeba ama watoto wawili au watatu wafike shule.

Mzazi anaweza akawa anakimbia gharama za shule na kukimbilia gharama za chini za bodaboda, lakini mwisho wa siku gharama ndogo inaweza inachangia gharama na madhara makubwa zaidi ya tiba na simanzi.

Hapo ndipo ninawasihi wazazi wenzangu wajaribu kuwafuatilia hao 'mabodaboda' wanasafirisha watoto wenu, mkiwa na kiulizo cha usalama wa huduma, hasa pale wanapobeba mtoto zaidi ya mmoja katika bodaboda zao.

Inawezekana kabisa, mzazi ukahisi bodaboda anamchukua mwanao peke yake na yuko usalama, kumbe alicho nacho nyuma ya pazia, ni balaa yenye viasharia vyote vya ajali kwa mtoto. Mungu aepushe mbali hili, hebu tuweni makini na hili jamani!

## Katibu Mkuu ataka ufumbuzi vikwazo utekelezaji wa bajeti

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KATIBU Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Juma Mkomi, amewataka wajumbe wa baraza la wafanyakazi la ofisi hiyo kuainisha na kuzitafutia ufumbuzi changamoto zitakazokwamisha utekelezaji wa bajeti ya ofisi kwa mwaka 2023/24 inayotarajiwa kuidhinishwa na Bunge.

Kwa kufanya hivyo, amesema itasaidia kuboresha huduma kwa wananchi na wadau wa masuala ya kiutumishi na utawala bora kama ilivyokusudiwa na serikali.

Mkomi alitoa maelekezo hayo juzi wakati akiongoza mkutano maalum wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora uliofanyika kwa lengo la kupitia taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2022/23 na mpango na bajeti kwa mwaka 2023/24.

Alisema kila mwaka bunge huidhinisha bajeti lakini wakati wa tathmini upungufu unabainika katika utekelezaji, hivyo aliwasihi wajumbe wa baraza kuainisha na kuzitafutia ufumbuzi changamoto zinazoweza kukwamisha utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/24.

"Ni wajibu wa kila mjumbe wa baraza hili kutoa mapendekezo yatakayowezesha utekelezaji wa bajeti yetu kwa mwaka wa fedha 2023/24 pindi Bunge litakapoidhinisha," alisisitiza.

Pia alisema ushirikiano wa kiutendaji chini ya uongozi wake ni suala analolipa kipaumbele ili kufikia azma ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuujenga utumishi wa umma unaowajibika kwa wananchi katika kutoa huduma bora.

Mkomi pia alitoa wito kwa wajumbe wa mkutano huo maalum kumshirikisha iwapo wana wazo au jambo ambalo wanafikiri likitekelezwa litakuwa na tija katika kuuboresha utumishi wa umma.

Aliongeza kuwa suluhu ya kuboresha utendaji kazi wa watumishi wasiowajibika si kuwahamisha vituo vya kazi bali waajiri wahakikishe wanarekebisha mapungufu yao ili waendelee kutoa huduma katika vituo vyao vya kazi alivyopangiwa.

"Hata kwenye ofisi yetu, kama kuna mtumishi ana hawajibiki ipasavyo sitamhamisha kwa sababu itatafsiriwa kuwa nimempeleka mtu mwenye tatizo eneo lingine ili akaharibu, hivyo niwahakikishie kuwa mtumishi atakayehama ni yule mwenye utendaji mzuri ambaye atatoa mchango kiutendaji katika taasisi nyingine." Alisema.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2022/23 na mpango na bajeti kwa mwaka 2023/24, Mtakwimu Mkuu Ofisi ya Rais - Utumishi, Ibrahim Kalengo, alisema serikali imeendelea kuunganisha mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) katika taasisi ili kubadilishana taarifa na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

Kalengo alitolea mfano wa mfumo shirikishi wa taarifa za kiutumishi na mishahara kuunganishwa na mifumo ya Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), mikopo ya elimu ya juu, Ajira Portal na mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).



Kaimu Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na Kati wa Benki ya CRDB, Bonaventure Paul (kushoto waliokaa) na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya usafirishaji mizigo ya Silent Ocean, Salah Mohammed, wakitiliana saini hati ya makubaliano jijini Dar es Salaam juzi, ya kuwawezesha wafanyabiashara wanaoagiza bidhaa kutoka nje ya nchi kupitia kampuni hiyo, kupata mkopo wa riba nafuu kwa kipindi cha kuanzia mwezi mmoja hadi miezi sita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NEMC yatoa darasa utokomezaji mifuko plastiki

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limeshiriki maonyesho ya Kimataifa ya Kilimo na Mazingira (Agriteq Expo 2023) katika jiji la Doha, Qatar na kuonesha uzoefu wake wa masuala mbalimbali ikiwamo utokomezaji wa mifuko ya plastiki.

Maonyesho hayo yalifanyika kuanzia Machi 15 hadi 19, mwaka huu na yalifunguliwa na Waziri wa Manispaa, Dk. Abdullah bin Abdulaziz bin Turki Al Subaie.

Akizungumza wakati wa maonyesho hayo, Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma wa NEMC, Irene John, alisema maonyesho hayo yatafungua fursa nyingi za uwekezaji katika bidhaa na huduma kupitia mawasilisho yaliyofanywa na NEMC imeonyesha mazingira ya uwekezaji yameboreshwa.

Alisema miongoni mwa mawasilisho ni pamoja na namna Tanzania ilivyoondoa mifuko ya plastiki na kutumia mifuko mbadala ambayo ni rafiki wa mazingira.

Pia alisema mazingira ya uwekezaji yameboreshwa kupitia mifumo mbalimbali ya kielektroniki kama vile mchakato wa utoaji vibali vya tathimini ya athari kwa mazingira na pia mfumo wa upatikanaji wa vibali vya taka hatarishi.

"Miongoni mwa wageni waliotembelea banda la NEMC ni pamoja na watumishi kutoka Ubalozi wa Tanzania nchini Qatar, wizara na kampuni mbalimbali kutoka nchi washiriki, mwananchi mmoja mmoja kutoka Qatar na nchi mbalimbali walitembelea pamoja na wawekezaji wa aina mbalimbali ili kupata elimu pamoja na kuelezwa fursa za uwekezaji kwenye mazingira, utalii na kilimo," alisema.

Kadhalika, Ofisa Mazingira kutoka NEMC Kanda ya Kusini, Obasanjo Nniwako, alisema moja ya faida kubwa kwa NEMC kushiriki katika maonyesho ya kimataifa ya mazingira na kilimo ni pamoja na kuitangaza NEMC na kutoa elimu juu ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira kwa uwekezaji endelevu.

"Lakini pia tumeeleza jinsi Tanzania ilivyotokomeza matumizi ya mifuko ya plastiki na kuonyesha kwa vitendo baadhi ya mifuko mbadala inayotumika ambayo ni rafiki kwa mazingira kwa ajili ya maendeleo endelevu kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo," alisema.

Naye Tilisa Mwambungo, Ofisa Mazingira toka Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, alisema kwenye maonyesho wanatangaza fursa za uwekezaji hasa katika kilimo endelevu kinachozingatia uhifadhi wa mazingira na utalii kwa ajili ya kukuza uchumi wa nchi na kuongeza ajira.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Vituo vya maji asilimia 34 vyabainika havifanyi kazi

**Na Beatrice Shayo**

ASILIMIA 34 ya vituo vya maji vijijini havifanyi kazi licha ya Tanzania kuandikisha asilimia 86 ya upatikanaji wa maji, kwa mujibu wa uchambuzi uliofanywa na Shirika la WaterAid.

Uchambuzi huo umefanywa katika nchi za Afrika Mashariki na Ethiopia eneo ambalo shirika hilo linafanya shughuli zake limebaini kuwapo kwa hali ya kutisha kuhusu menejimenti ya majisafi na usafi wa mazingira.

Uchambuzi huo unaonyesha kuwa zaidi ya nusu ya vituo vya afya nchini Tanzania, havijaunganishwa na huduma ya bomba ya majisafi na salama.

Hayo yalibainika wakati wa mkutano uliofanyika mwishoni mwa wiki kuelekea kilele cha maadhimisho ya Siku ya Maji Duniani (WWD). Kwa mwaka huu, WWD itaadhimishwa Machi 22, 2023, ikiwa na kaulimbiu, 'Kuongeza kasi ya upatikanaji wa maji katika kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa'.

Akifungua mkutano huo, Mkurugenzi wa WaterAid Kanda ya Afrika Mashariki na Ethiopia, Olutayo Bankole-Bolawole, alisema Tanzania imefanikiwa kuandikisha mafanikio ya upatikanaji wa maji kwa asilimia 86.

"Hata hivyo, asilimia 34 ya vituo vya kutolea huduma hiyo vilivyoko kwenye jamii za wananchi waishio vijijini havifanyi kazi na nusu ya vituo vya afya vikiwa havijaunganishwa na huduma ya maji ya bomba," alisema.

Bankole-Bolawole alisema uchambuzi huo unaonyesha kuwa nusu ya wakazi nchini Ethiopia wanapata huduma ya majisafi ya kunywa.

"Nchini Rwanda, asilimia 45 ya wananchi wanakosa huduma za msingi za maji na asilimia 56 ya wananchi nchini Uganda wanapata angalau huduma za kimsingi zinazohusiana na maji," alisema.

Aidha, alisema idadi ya watu duniani wanaotumia majisafi ya kunywa iliongezeka kutoka asilimia 70 mwaka 2015 hadi 74 mwaka 2020.

Alisema watu bilioni mbili hawapati huduma hizo, wakiwamo bilioni 1.2 ambao walikosa huduma za kusambaziwa maji.

Alisema dunia itafikia asilimia 81 ya usambazaji maji ifikapo 2030 na kutofikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) huku watu bilioni 1.6 wakiachwa bila menejimenti ya usambazaji salama wa maji ya kunywa.

Bankole-Bolawole alisema lengo la Maendeleo Endelevu (SDG) namba sita, dunia iliazimia mwaka 2015 kila mtu atapata maji na huduma za usafi zinazosimamiwa kwa usalama ifikapo mwaka 2030.

Hata hivyo, alisema wanawake na wasichana ndiyo wanaoathirika zaidi kwa kulazimika kutembea umbali mrefu kutafuta maji na kukosa fursa za elimu na ajira hali inayosababisha kushamiri kwa mzunguko wa umaskini na kukwamisha ukuaji wa uchumi wao.

Alisema nchi za Afrika Mashariki na Ethiopia ziko katika hatari kubwa ya athari za mabadiliko ya tabianchi na hali mbaya ya hewa inayosababisha ukame na tatizo la usalama wa chakula.

Katika mkutano huo, washiriki toka Uganda, Kenya, Tanzania, Rwanda na Ethiopia walijadili umuhimu wa ushirikiano utakaowezesha upatikanaji endelevu wa maji salama na usafi wa mazingira katika ukanda huo.

Alisema uhaba wa maji unasababisha changamoto mbalimbali ikiwamo magonjwa ya milipuko, migogoro, ukosefu wa chakula, kuhama makazi kuongezeka kwa usawa na vifo vya mama na mtoto.

Nelson Gomonda, alisema Afrika inatarajiwa kuwa na ongezeko kubwa la watu na kwamba ni muhimu kuwapo kwa usimamizi bora wa rasilimali za maji ili kuepusha hatari na mashaka katika siku zijazo.

"Afrika nje ya malengo katika kufikia SDGs hasa SDG 1 na 2 kufikia mwaka 2030. Ufadhili wa miradi toka nje haujasaidia ipasavyo utekelezaji wa programu za maji hivyo tunapaswa kubadilika katika eneo hilo," alisema.

Kwitunda Philippe kutoka Rwanda alisema kulinda rasilimali za maji ni suala muhimu litakaloifanya Afrika Mashariki na Ethiopia iwe na maji endelevu kwa watu wake.




Ofisa Mkuu wa Tigo Pesa, Angelica Pesha (katikati), akizungumza wakati wa uzinduzi wa kadi mtandao ya Tigo Pesa Mastercard jijini Dar es Salaam juzi. Wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa Selcom, Sameer Hirji (kulia) na Mwakilishi kutoka Mastercard, Oyuga Lenin. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wabunge wanawake EALA watembelea CCBRT

**Na Mwandishi Wetu**

WANAWAKE wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA) wameitembelea Hospitali ya CCBRT kujionea shughuli na huduma zinazotolewa katika hospitali hiyo.

Mbunge wa Afrika Mashariki anayewakilisha Tanzania, Dk. Shogo Sedoyeka, alisema ziara hiyo iliandaliwa na mwanzilishi na Ofisa Mtendaji Mkuu wa taasisi isiyo ya kiserikali 'Fungua Trust'.

Wabunge hao walikuwa Dar es Salaam kwa shughuli za Kamati ikizijumuisha Kamati za Kudumu za Kilimo, Utalii na Maliasili na Sheria, Kanuni na Stahili na pia katika maadhimisho ya Siku ya Mwanamke Duniani.

Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Hospitali ya CCBRT, Brenda Msangi, aliwatembeza katika vitengo mbalimbali kikiwamo kipya na cha kisasa cha afya ya uzazi kilichofunguliwa Julai, 2022 na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na kupewa jina lake.

Alisema pia hospitali hiyo hutoa matibabu kwa wagonjwa kutoka ndani na nje ya nchi kwa kuzitaja baadhi ya nchi ambazo mara nyingi hupokea wagonjwa wake kuwa ni Comoro, Msumbiji, Malawi na Yemen.

Walitembelea wagonjwa wa fistula ambao hupatiwa ya mafunzo ya ujasiriamali na hospitali hiyo.

Walifurahishwa na hospitali hiyo inavyojenga ujuzi kwa wafanyakazi wake wa ndani na kutoka taasisi na kampuni mbalimbali kuhakikisha kuwa Tanzania ina rasilimali watu wenye uwezo unaohitajika kutoa huduma bora kupitia kitengo chake cha Mafunzo (CCBRT Academy).

Brenda alieleza mifumo mbalimbali ya kuongeza utendaji na uwajibikaji na udhibiti rasilimali za taasisi hiyo. Pia alisema wanavyosaidia jamii kutoa matibabu ya bure kwa kubuni njia mbalimbali za kugharimia matibabu hayo pamoja na kufanya kazi kwa karibu na serikali na wadau mbalimbali wa maendeleo.

Naye mheshimiwa Balozi Fatuma Ndangiza ambaye ni Katibu Mkuu wa Umoja huo wa wanawake wa Bunge la Afrika Mashariki alisema; "Ninakupongeza Mtendaji Mkuu kwa usimamizi mzuri wa uendeshaji mzuri wa shughuli za hospitali hii," alisema.

"Sisi kama wabunge tumeona na kujifunza mambo mengi ambayo yameongeza uelewa wetu wa masuala mbalimbali na changamoto zinazowakabili wanawake na watoto na tutatumia nafasi zetu kuleta maboresho ya kisheria na kisera ili kuendana na mazingira ya sasa ya ukuaji wa teknolojia na ubunifu ili kupunguza changamoto hizo na kuongeza ushiriki wa jamii katika shughuli za kiuchumi ndani ya Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki."

Taasisi ya Fungua imeanzishwa nchini Tanzania ikiwa na lengo la kujenga uwezo wa jamii kutumia fursa zilizopo katika maeneo yao ili kuinua hali zao za maisha.

# TEN/MET yazindua mpango mkakati wa elimu miaka mitano

**Na Elizabeth Zaya**

MTANDAO wa Elimu Tanzania (TEN/MET) umezindua mpango mkakati wa elimu wa miaka mitano kuanzia mwaka huu, hadi 2027 huku zaidi ya wanafunzi milioni 27 wakitarajiwa kunufaika katika mpango huo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mpango huo jijini Dar es Salaam juzi, Mratibu wa Taifa wa Mtandao huo, Ochola Wayoga, alisema wanatarajia utasaidia kuongeza ufanisi katika sekta hiyo.

Alisema mpango mkakati huo unagusa masilahi ya walimu, namna wanavyofundisha husan katika madarasa ya wanafunzi wengi na mbinu mpya za ufundishaji.

"Na tunaamini kwamba kupitia mpango mkakati huu, kila Mtanzania apate elimu bora na hata kuongeza rasilimali za elimu kwa sababu bajeti ya elimu haijatimia asilimia 20 ya bajeti yote katika sekta hiyo na kwa kushirikiana na serikali kupitia mpango huu tunatarajia ndani ya miaka mitano nchi yetu itakuwa na uwezo wa kuwekeza asilimia hiyo ya bajeti nzima," alisema Ochola.

Alisema wanatarajia kwenye mpango mkakati huo ni kuimarisha maadili katika sekta ya elimu.

"Mpango mkakati unakwenda kukuza maisha ya maadili ya vijana katika ngazi zote za elimu kuanzia shule ya msingi mpaka vyuo vikuu. Tunataka wawe na maadili na ambao wanaweza kujitawala na kufanya maamuzi yatakayowasaidia kuendeleza nchi yetu."

Suala la uchumi wa taifa ni miongoni mwa mambo yanayotarajiwa kuboreshwa na mpango mkakati huo.

"Kwa sababu tunatarajia vijana wakimaliza shule watajiajiri na kuajiri wengine, watakuwa wabunifu na watakuwa ni rasilimali ya kutegemewa na taifa. Kila kitakachofanyika kwenye mpango huu lazima kitagusa maisha ya wanafunzi ngazi zote na tunatarajia wanafunzi milioni 27 watanufaika kwa miaka mitano," alisema.

Alisema wanatarajia mpango mkakati huo utakuwa jumuishi unaotarajia kutumia Sh. bilioni 20 kwa kipindi cha miaka mitano.

Mdhibiti Ubora Elimu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Ephraim Simbeye alisema wanaamini mpango mkakati huo umekuja kwa wakati muafaka na utachangia jitihada zinazofanywa na serikali za kuboresha sekta ya elimu nchini.

Alisema serikali inatambua na kuthamini mchango mkubwa unaofanywa na wadau hao katika kuboresha sekta hiyo nchini na itaendelea kushirikiana nao katika kuiboresha zaidi.





## Ujenzi soko la madini Mirerani kujengwa usiku, mchana

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

MKURUGENZI Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Hamad Abdalah, amesema mradi wa ujenzi wa soko la madini katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani utafanyika mchana na usiku ili ukamilike kwa wakati kama ilivyopangwa.

Alitoa maelezo hayo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii iliyokwenda Simanjiro kukagua utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa soko hilo.

Hamad alisema kwa kuzingatia jitihada kubwa ambazo zinafanywa na Rais Samia Suluhu Hassan, watajitahidi kufanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha jengo hilo linakamilika kwa wakati na ubora unaotakiwa.

Vilevile alisema mradi huo ulianza Mei 22 mwaka 2022 unatarajiwa kukamilika Mei 21 mwaka huu kwamba jengo hilo la ghorofa tano litaigharimu Sh.bilioni 5.4.

"Katika mchakato mzima wa ujenzi tumekumbana na baadhi ya matatizo ikiwamo upandaji wa bei ya vifaa mara kwa mara na uwapo wa mvua kubwa ulioathiri kasi ya utekelezaji wa ujenzi wa mradi," alisema Abdalah.

Aidha, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geofrey Pinda, alisema kujengwa kwa soko hio katika eneo hilo kutaondoa hofu ya baadhi ya watu waliodhani soko la madini litahamishwa Mirerani.

Katika ziara hiyo, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Simanjiro, Kiria Laizer, aliishukuru serikali kwa ujenzi wa jengo hilo kwenye eneo hilo akisema litaongeza uchumi kwa wananchi wa Simanjiro. Baada ya maelezo hayo, Mjumbe wa kamati hiyo, ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum (Vijana Taifa), kupitia Mkoa wa Manyara, Asia Halamga, aliiomba serikali kutoa fedha kwa wakati ili kukamilisha jengo hilo.

"Fedha zikifika kwa wakati jengo litakamilika kwa muda uliopangwa, pia nawapongeza Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere na Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Dk. Suleiman Serera kwa kufuatilia kwa karibu ujenzi wa mradi wa jengo hili hadi ulipofikia," alisema Halamga.

Kadhalika, alisema jengo hilo likikamilika litaongeza hadhi na thamani ya Mji wa Mirerani kwa kuwa na utajiri mkubwa wa madini ya tanzanite ulioko kwa kuwa watu wengi wamewekeza nje ya eneo hilo.

# Mbunge aishauri h/shauri kurasimisha makazi Mirerani

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

MBUNGE wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara, Asia Halamga, ameishauri Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, kurasimisha makazi ya watu 978 walioko Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani.

Wananchi hao ni wale walilipa Sh.250,000 kila mmoja tangu mwaka 2019 kwa ajili ya kupimiwa viwanja vyao.

Halamga ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii alitoa ushauri huo juzi baada ya kamati hiyo kuitembelea mamlaka hiyo.

Mbunge huyo alisema wananchi 978 wa eneo hilo hawatambui hatima ya fedha zao, kwa kuwa kila mmoja alitoa Sh.250,000 ili wapimiwe makazi lakini kazi hiyo haikufanyika.

"Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, mnapaswa kujibu hili kwa kuwa wananchi hawa wa Mirerani wamelalamikia hili kwa muda mrefu,"alisema.

Hata hivyo alisema serikali wilayani humo inapaswa kutoa majibu ni lini wananchi hao, watatimiziwa hitaji lao kwa kuwa wameshalipa fedha kwa ajili ya kupatiwa huduma.

Akitoa ufafanuzi wa jambo hilo Kamishna Msaidizi wa Ardhi wa Mkoa wa Manyara, Wenceslaus Mtui, alisema kati ya watu hao 978 wanaohitaji huduma hiyo ni 47 pekee walilipa fedha hizo.

Vilevile alisema kati ya watu ni 30 pekee waliolipia Sh.250,000 na wengine 17 waliobaki walilipa Sh.150,000.

"Mwaka 2020 Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi alitoa waraka wa kupunguza upimaji kutoka Sh.250,000 hadi kufikia Sh.150, 000 zinazolipwa kwa sasa," alisema Mtui.

Aidha, alisema Halmashauri ya Wilaya hiyo, ilibidi itoe fedha zake za mapato ya ndani Sh.milioni 50 kwa ajili ya shughuli hiyo ambayo baadhi wameshapatiwa hati za viwanja.




Meneja wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB) Tawi la Musoma, Hagai Gilbert (kulia), akikabidhi sehemu ya msaada wa mabati 135 kwa Diwani wa Kata ya Hunyari, Mugungi Muhochi, yaliyotolewa na benki hiyo jana, kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa zahanati ya kijiji cha Nyamikoma wilayani Butiama. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makusanyo ada ya utalii yaingizia taifa bil.24.9/-

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKOA wa Manyara umeliingizia taifa zaidi ya Sh. bilioni 24.9 zinazotokana na makusanyo ya ada ya utalii katika kipindi cha miaka miwili ya utawala wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Mkuu wa Mkoa huo, Makongoro Nyerere, aliyasema hayo juzi na kueleza kuwa idadi ya watalii walioliingizia taifa mapato hayo ni 276,832.


"Watalii hao ni wale walioingia nchini na kutembelea Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na Hifadhi ya Taifa ya Manyara. Katika kipindi hicho, pia serikali imetoa Sh.bilioni 2.7 kwa ajili ya maboresho ya mazingira ya utalii kwenye Hifadhi ya Taifa ya Tarangire ili fedha hizo zisaidie ujenzi wa kiwanja cha ndege ndani ya hifadhi hiyo." alisema.

Kwa mujibu wa Makongoro uwanja huo wa ndege utajengwa kwa kiwango cha moramu ili kuwarahisishia watalii kufika kwenye hifadhi hiyo na kupunguza muda wa kutumia usafiri wa magari.

Mbali na utalii katika kipindi hicho Mamlaka ya Mapato nchini (TRA), ilikusanya Sh. bilioni 64.3, tofauti na kipindi cha nyuma ambacho walikuwa wakikusanya zaidi ya Sh. bilioni 40.

Alisema katika makusanyo ya mapato ya halmashauri za wilaya kwa kipindi hicho zilikusanya Sh. bilioni 25.6.

Alizitaja sababu za kufanya vizuri kwenye eneo la mapato kwa TRA na halmashauri ni pamoja na kufanikiwa kuzuia vikosi kazi na kuongeza hamasa kwa wafanyabiashara na walipa kodi kulipa kodi kwa hiari.





# TCB yatoa msaada mabati 135 ujenzi wa zahanati

**Na Mwandishi Wetu,** MUSOMA

BENKI ya TCB imetoa msaada wa mabati 135 yatakayotumika katika ujenzi wa zahanati katika Kijiji cha Nyamkoma kilichoko wilayani Butiama mkoani Mara.

Msaada huo ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za serikali katika kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma ya afya, ulipokelewa na Diwani wa Kata ya Kinyare, Mkingi Itagata.

Akipokea msaada huo, diwani huyo alisema bado kuna uhitaji ili ukamilisha ujenzi wa kituo hicho cha afya kwani gharama ya ujenzi ni Sh. milioni 150 lakini hadi sasa kiasi walichokusanya ni Sh.milioni 47.

"Serikali pamoja na wazazi tutaongeza nguvu kwenye ujenzi huu maana wananchi wamekuwa wakifuata huduma ya afya mbali kidogo na kijiji hicho," alisema Mingi.

Akizungumza baada ya kukabidhi msaada huo, Meneja wa Benki ya TCB Tawi la Musoma, Gilbert Hagai, aliwahakikishia wananchi wa kijiji hicho kuwa TCB itaendelea kuunga mkono juhudi za wananchi wapenda maendeleo na kuhakikisha kuwa benki hiyo inasogeza huduma zake karibu.

Aidha, aliwapongeza wazazi na uongozi wa kijiji kwa jitihada za kuchangia na kuanza ujenzi wa zahanati hiyo toka mwaka 2017, kwamba imeonyesha kuwa ni kwa namna gani kumekuwa na uhitaji.

Alisema: "Benki yetu ni mdau mkubwa wa maendeleo kwa kawaida kila mwaka tunatenga fungu kutoka katika faida yetu kwa ajili ya kurudisha katika jamii na tunaipa kipaumbele kwani kuwekeza kwenye elimu, afya na maeneo mbalimbali tukiwa kama benki tunaamini vitu hivi vyote vinatusaidia kupata wateja na wafanyakazi wa benki yetu wa baadaye."

Alisema wataendelea kuchangia na kuunga mkono juhudi za serikali katika kuboresha sekta ya afya kwa kadri watakavyoweza na kusema kwamba kwa kutoa msaada huo siyo mwisho kwa wao kutoa misaada.

# Sababu kesi za ukatili, ndoa za utotoni 'kuyeyuka' zatajwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga limetaja sababu zinazosababisha kesi nyingi za vitendo vya ukatili wa kijinsia, ndoa za utotoni kushindwa kufikia hukumu kuwa ni ukosefu wa nyumba ya kuhifadhia waathirika wa ukatili huo pamoja na sheria kinzani.

Hayo yamebainishwa na Mkuu wa Dawati la Jinsia kutoka Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Monica Sahere, wakati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mradi wa kupinga ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Alisema kinachoendelea kuzuia wahusika waliowapa mimba watoto kufungwa jela ni ukosefu wa ushahidi, hali inayosababishwa na ukosefu wa nyumba ya kuhifadhia waathirika hao.

Sahere alisema sababu wakirudi nyumbani wazazi wao huwarubuni kuwakana watuhumiwa na kumalizana kimya kimya.

"Hili la kuharibu ushahidi ambapo inapaswa iwapo nyumba maalumu kwa ajili ya kuwahifadhi waathirika hadi kesi itakapokwisha wasirudi nyumbani kwao ili wahusika wafungwe jela," alisema Sahere.

Ofisa Operesheni kutoka Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Emmanuel Galiyamoshi, akizungumza kwa niaba ya Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani humo, Janety Magomi, alisema uwepo wa nyumba ya kuhifadhia waathirika wa mimba na ndoa za utotoni itasaidia kwa kiasi kikubwa kutoharibu ushahidi sababu watoto hao watakuwa mbali na wazazi wao.

Alisema Jeshi la Polisi tayari limeanza kutekeleza mpango huo wa kujenga chumba cha kuhifadhia waathirika wa matukio ya ukatili, kwamba katika Kituo cha Polisi wilayani Kishapu kuna chumba kimoja kimetengwa kwa ajili ya kuwahifadhi kwa muda, ili wasiwe karibu na wazazi wao na kurubuniwa na wahusika au kutoroshwa na hatimaye ushahidi kukosekana.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Joram Magana, alisema mashirika yasiyo ya kiserikali, Jeshi la Polisi pamoja na waandishi wa habari, wamekuwa na mchango mkubwa wilayani humo kupunguza matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto zikiwamo mimba na ndoa za utotoni.

Alisema matukio ya ukatili yamepungua kutokana na wananchi kupewa elimu ya madhara ya ukatili na wamekuwa wakitoa taarifa za ukatili zikiwamo harusi za ndoa za utotoni.




Wanafunzi wa Shule ya Msingi Gilime, Kata ya Kilago, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, wakiwa wamekalia sehemu ya madawati 500 yenye thamani ya Sh. milioni 60, yaliyotolewa na Shirika la World Vision Tanzania jana ili kupunguza changamoto ya uhaba wa madawati shuleni. **PICHA: SHABAN NJIA**

# SBL yajizatiti kusaidia jamii huduma ya majisafi, salama

**Na Vitus Audax,** MWANZA

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) imesema itaendelea kutoa msaada wa huduma ya majisafi na salama kwa jamii kupitia miradi mbalimbali pamoja na kulinda vyanzo vya maji.

Meneja wa Mawasiliano na Mambo Endelevu wa SBL, Rispa Hatibu, aliyasema hayo jana jijini hapo wakati wafanyakazi wa kampuni hiyo waliposhiriki kufanya usafi katika Mto Miringo unaopeleka maj i Ziwa Victoria.

Hatibu alisema kampuni hiyo iko tayari kuendelea kuwekeza kwenye juhudi za kulinda vyanzo vya maji sambamba na kauli mbiu ya Siku ya Maji Duniani isemayo 'kuongeza mabadiliko kupata suluhisho la mgogoro wa majisafi'.

Kazi ya kufanya usafi katika mto huo ilifanywa na wafanyakazi wa SBL kwa kushirikiana na wa Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Victoria.

Hatibu alisema SBL imefanikisha mambo mengi yanayohusiana na huduma za maji na utunzaji wake ikiwamo miradi mikubwa 24 ya maji nchini katika kipindi cha miaka 10 iliyonufaisha wakazi milioni mbili kupitia programu iitwayo 'water for life'.

"SBL itaendelea kushirikiana na wadau wengine kuwezesha jamii zenye uhitaji wa majisafi na salama kupata maji. Hii ni ahadi tuliyojiwekea chini ya mpango kazi wetu tunaouita 'society 2030,'' alisema Hatibu.

Machi mwaka huu SBL iliwekeza Sh.milioni 380 kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa bwawa la maji la Kwamizi lililopo wilayani Handeni mkoani Tanga.

ama
ALHAMISI MACHI 23, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Vita ndoa za utotoni ilivyochachamaa**



Ukurasa 13

**USHUHUDA WA MADHARA...**
Kuvulia nyavu plastiki kunavyoua kundi la samaki, viumbe kutoweka




Ukurasa 14

**Ilivyo vita vya kukabili kasi HIV, dawa kulevya Mwanza**

ZAMA AWAMU YA SITA...

# Ofisi Makamu Rais yaanika hatua zake katika mazingira

• Safari imeanza mkakati 2022 -32

**Na Mwandishi Wetu**

ILIKUWA tarehe 6 Novemba mwaka jana, kulikuwapo kikao cha kamati ya pamoja ya Serikali ya Muungano na ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kilichofanyika jijini Dodoma kilichojadili hoja nane za Muungano, nne ambazo ni nusu ya idadi hiyo, zikipatiwa ufumbuzi na kuondolewa kwenye orodha hiyo ya Muungano.

Hizo zilizoondolewa zinajumuisha; malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili na Kodi ya Mapato (PAYE) na Kodi ya Zuio (Withholding Tax).

Pia, kuna suala la kuongezeka gharama za umeme kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwenda Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO); pia Mkataba wa Mkopo wa Fedha za Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (Terminal III). Sasa zimefanyiwa kazi na rasmi zimeondoewa kwenye kero hizo.




Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, akizindua mpango kuuza hewa ya ukaa. **PICHA: MTANDAO**

### ULINGO WA MAZINGIRA

Inapotajwa mamlaka inayosimamia mazingira kitaifa, Ofisi ya Makamu wa Rais, ndiko alikotokea Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, huko akiwa Makamu wa Rais akisimamia moja kwa moja Muungano na Mazingira.

Mbali na miaka miwili ya urais wake sasa, zama hizo ndani ya miaka sita iliyopita, ndiye aliyeandaa misingi ya yote yanayoamuliwa sasa, akiwa mkuu wa nchi kwa miaka miwili.

Mnamo Februari 12, 2021 Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, alizindua Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 jijini Dodoma inayojumuisha mapya, yakiwamo udhibiti wa taka za kielektroniki, pia kusimamia na kutumia kemikali.

Mengine yanayotajwa ni kudhibiti uchafuzi katika shughuli za kutafuta na kuchimba mafuta na gesi, mabadiliko ya tabianchi, kusimamia matumizi salama ya baioteknolojia ya kisasa na udhibiti wake.

Lengo hapo linatajwa ni kuongeza kiwango cha ushiriki wa wadau katika kuhifadhi mazingira, hali kadhalika kuongeza chachu ya kutekeleza mikakati ya kusimamia mazingira, akishirikisha wajumbe kutoka sekta binafsi na asasi za kiraia, wanaounda Kamati Maalum ya Uratibu na Mabalozi wa Mazingira wanaoshiriki katika uhamasishaji.

### SERA & MPANGO

Ofisi ya Makamu wa Rais, imeandaa Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 - 2032), ambao ukazinduliwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, katika kilele cha Siku ya Mazingira Duniani, Juni 5, mwaka jana, jijini Dodoma, unaotekelezwa kwa kipindi cha miaka 10.

Mpango huo unaainisha changamoto za kimazingira na mikakati ya kukabiliana nazo, kwa kuzingatia tofauti za maeneo mbalimbali nchini.

Katika maudhui yake, kuna masuala yanayoainishwa kama vile; uharibifu wa ardhi, pua vyanzo vya maji, athari za mabadiliko ya tabianchi, kuchafuliwa mazingira, miti kukatwa ovyo na uharibifu wa misitu.

Changamoto nyingine inatajwa ni kupotea kwa makazi ya wanyamapori na bioanuai yake, kuharibika kwa mfumo- ikolojia kwenye pwani na baharini, uharibifu wa ardhi oevu, usimamizi hafifu wa taka, kuenea kwa viumbe vamizi na changamoto za mazingira katika miji.

Ni mtazamo ambao mkakati huo, unalenga kuupatia ufumbuzi changamoto tajwa, Mpango Kabambe ukiainisha hatua za kimkakati na mahsusi, zinazozingatia jiografia na mifumo ikolojia ya maeneo husika.

### MWONGOZO WA KABONI

Biashara ya kaboni, inatajwa kuingia katika orodha ya nyenzo muhimu katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi duniani ambayo inafanyika miongoni mwa nchi wanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi, Itifaki ya Kyoto na Makubaliano ya Paris.

Kwa kuzingatia hilo serikali imeandaa kanuni na Mwongozo wa Taifa wa Usimamizi wa Biashara ya Kaboni, lengo ni kuweka utaratibu na masharti, ambayo wadau na wajasiriamali wa biashara ya kaboni watapaswa kuzingatia.

Inafafanuliwa, hilo linafanyika wakati wa utekelezaji wa miradi mipya inayoendelea ya biashara ya kaboni katika sehemu mbalimbali ndani ya Muungano wa Tanzania.

Hadi sasa inafafanuliwa, katika

**INAENDELEA UK.12**

AFYA

# Vita ndoa za utotoni ilivyochachamaa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA



Mama kijana akimhudumia mwanawe. **PICHA: MTANDAO**

KISHERIA, mtoto anaangukia umri wowote anapokuwa chini ya miaka 18, hivyo hana fursa kisheria kufunga ndoa.

Hata hivyo, kurejea na uhalisia bado kuna tatizo kubwa watoto wa umri huo kuendelea kufungishwa ndoa na hasa maeneo ya vijijini.

Msukumo mkubwa wa matukio hayo, inaelezwa ni shinikizo la mila, desturi na utamaduni potofu wa baadhi ya makabila kwa tamaa ya kupata mali na hususani mifugo. Mara zote, mhanga huwa binti anayeozeshwa kwa mwanaume anayemzidi umri.

Wasichana kutoka familia zenye kipato duni, ndio zaidi wanaangukia uwezekano mkubwa kuolewa kabla ya kufikisha umri miaka 18, ikilinganishwa na watokao katika familia zenye kipato cha juu, kwa maana wanaoishi pembezoni mwa miji, huangukia ukatili huo.

Utafiti wa Demografia ya Afya nchini( TDHS) wa mwaka 2010, unaonyesha mkoa wa Shinyanga unaongoza kwa ndoa za utotoni, ikiwa na wastani wa asilimia 59 ya ndoa zake, ikifuatiwa na Tabora asilimia 58; Mara asilimia 55 na Dodoma asilimia 51. Maana yake ni kuwa kundi la wasichana watano, wawili kati yao huolewa kabla ya muda wao.

Katika hali ya kulitatua hilo, wavulana katika Shule ya Msingi Shilela na Sekondari ya Nyikoboko katika Halmashauri ya Msalala, mkoani Shinyanga, wakaamua kujitwisha jukumu la kutoa taarifa za ukatili wanaofanyiwa wanafunzi wenzao wanaoozeshwa katika umri mdogo, kuhakikisha wanatimiza ndoto zao.

### WANENAVYO WANAFUNZI

Joseph (jina la pili tunalo), anayesoma kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Nyikoboko, anasema ndoa za utotoni ni kikwazo kwa wanafunzi wenzao wa kike kushindwa kutimiza ndoto zao, kwa tamaa za wazazi kutaka mali, ihali watoto wao ni wanafunzi.

Anasimulia mkasa, mwanafunzi mwenzao alipata ujauzito wakiwa kidato cha pili na akaacha masomo, hata kabla ya kufanya mtihani wa kuingia kidato cha tatu, akijifungua kwa njia ya upasuaji, mtoto yupo salama, lakini mama yake alipata maradhi mpaka sasa anahangaika.

Salumu (jina la pili tunalo), mwafunzi wa darasa la sita shule ya msingi Shilela anasema mwenzao alifaulu kujiunga na shule ya sekondari, lakini wazazi wake waligoma kumsomesha, wakidai hawana fedha za kumhudumia, kumbe walilenga kumuozesha. Wao walitoa taarifa polisi na mpango huo wa wazazi ukadhibitiwa kufanyika na sasa anaendelea na masomo.

Mwanafunzi Mathayo anayesoma kidato cha tatu, anasema, wakiwa kidato cha pili kuna mwanafunzi mwenzao wa kike alipata ujauzito na kukatisha masomo. Hivi karibuni walishiriki kwenye sherehe yake ya kutolewa mahari na ameolewa na mtu mzima.

"Sisi kwa sasa tumeingiwa na wasi wasi wa wanafunzi wenzetu wa kike kushindwa kuhitimu masomo yao, kwa kuendelea kupata ujauzito, tuwaombe mtandao wa jinsia Tanzania (TGNP) washirikiane na serikali, kutokomeza tabia hii inayokatisha ndoto za dada zetu," anasema.

### MIKAKATI ILIYOPO

Mwanafunzi Jonasi naye wa kidato cha tatu, anaeleza katika kukomesha vitendo hivyo, wamejipanga kuanzisha klabu shuleni, ambayo itakuwa inawakutanisha na kujadili yanayowakabili shuleni na nyumbani, hata wakazifikisha katika uongozi kwa msaada zaidi.

Anaahidi kuhakikisha wanatoa taarifa za walimu wasio waadilifu kutaka uhusiano na dada zao, nao watafikisha taarifa zao shuleni, pia kwa ofisa mtendaji wa kata na kituo cha polisi, washughulikiwe kisheria.

Shadia, anayesoma katika shule ya msingi, anataka elimu ya ukatili iendelee kutolewa shuleni kote, nao wazifikishe majumbani kwao, kwani wazazi na dada zao hawafahamu wapi pa kupeleka malalamiko yao.

### KUTOKA KWA MWALIMU

John Banda, Mwalimu wa Taaluma wa Shule ya Sekondari Nyiboko, anakiri kuwepo tatizo wasichana shuleni kupata ujauzito na kushindwa kuendelea na masomo, japo baadhi yao wamekuwa na uwezo mkubwa, akitoa mfano mwaka huu kumeripotiwa mkasa mmoja wa mwanafunzi kidato cha tatu kupata ujauzito.

Pia, anataja mwaka jana kuna mwanafunzi alifanya mtihani wa kidato cha pili akiwa mjamzito bila ya wao kujua na alifaulu kuingia kidato cha tatu, lakini alishindwa kuendelea, kwa sababu tayari alikuwa mjamzito.

Mwalimu Banda anasema, wamebuni mkakati wa kukutana na wanafunzi wote kila mwezi na kuwasikiliza matatizo yanayowakabili, kisha wanayatatua na yaliyo nje ya uwezo wao wanayafikisha kwa vyombo vya sheria, wahusika wawajibishwe.

Hapo, anaungwa mkono na Joseph Samweli, kutoka Kituo cha Taarifa na Maarifa Kata ya Shilela, ana nyongeza kila mwezi wamekuwa na utaratibu wa kutembelea kijiji kimoja na kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia, pia mimba na ndoa za utotoni wanazozibaini, wanaziripoti kwa Ofisa Mtendaji wa Kata.

### MTAALAMU WA TGNP

Mtaalamu wa Jinsia na Maendeleo, kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Hancy Obote, analalamika ukatili wa kijinsia haukubaliki, akifafanua:

"Toeni taarifa kwa viongozi wa serikali za mitaa, vituo vya taarifa na maarifa na viongozi mbalimbali wa serikali ili kukomesha vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto wadogo."

Ofisa Programu wa mtandao huo, Jackson Malangalila, anasema, kwa sasa wameshawafikia wanafunzi wa kiume 145 Shule ya Msingi Shilela, pia sekondari za Lunguya na

Nyikoboko, lengo ni kuwahusisha wavulana katika kutokomeza matukio ya ukatili wa kijinsia na kuwawezesha kuwa sehemu ya kuondoa ukatili huo.

Anasema mtandao huo unatekeleza mradi wa kuimarisha ushirikishwaji na uelewa wa jamii yahusuyo ukatili wa kijinsia na mila potofu kwa wanawake na watoto, katika Halmashauri ya Msalala - Shinyanga na Kasulu - Kigoma.

# Ofisi Makamu Rais yaanika hatua zake katika mazingira

**INATOKA UK.11**

miaka miwili nchi inapoongozwa na Rais Dk. Samia, kuna orodha ya mafanikian yanayotajwa katika eneo hilo, msingi mkuu wa upande mwingine wa mafanikio, ukitajwa jamii kuwa na umoja, katika pande mbili za Muungano.

"Ofisi (ya Makamu wa Rais) itaendelea kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi katika kutekeleza mipango, mikakati na programu mbalimbali za kuhifadhi mazingira kwa maendeleo endelevu,: inatamka taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

### MIKUTANO KIMATAIFA

Tangu Dk. Samia apitishwe kuwa Rais mwaka jana, bado ustawi wa ushiriki kimataifa katika masuala ya mazingira, umedumu kuwa endelevu.

Mnamo Novemba mwaka 2021, Tanzania imeshiriki katika Mkutano wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi, uliofanyika jijini Glasgow nchini Scotland na jijini Sharm El Sheikh nchini Misri, ambako Novemba mwaka jana, ilikofanyika .

Aidha, mwezi huu kulikuwa na mkutano wa kutetea na kuloimda mazingira barani Afrika, jijini Sharm El Sheikh, ukiwa ni mahsusi kwa ajili ya nchi zinazoendelea, ambako Makamu wa Rais Dk. Phillip Mpango, aliwakiliasha nchi, akiambata na mawaziro kadha wa pande mbili wa Muuungano.

Ni mara zote katika mikutano hiyo, Tanzania imeendelea kutoa wito kwa mataifa yaliyoendelea kutoa fedha za kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa nchi zinazoendelea, ikiwamo nchini.

Pia, Tanzania imetumia mikutano hiyo kuelezea mikakati ya serikali ya kuhifadhi mazingira, kupitia jukumu la kupandaji miti linalotekelezwa nchini, sambamba na kutungwa kanuni na miongozo inayoleta matokeo chanya kitaifa.

Matokeo hayo, ni pamoja na kuqwachagiza wawekezaji kutoka mataifa mbalimbali duniani, kuchangamkia fursa za kuwekezaji katika biashara ya kaboni nchini.

Ni aina ya mafanikio makubwa yaliyopatikana ndani ya kipindi cha miaka miwili ya Serikalo ya Awamu ya Sita yametokana na jamii yenye umoja, mshikamano na isiyo na ubaguzi.

**• Makala hii imeandaliwa kutokana na taarifa kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais.**

MAZINGIRA

## USHUHUDA WA MADHARA...

# Kuvulia nyavu plastiki kunavyoua kundi la samaki, viumbe kutoweka



Rais Samia Suluhu, alipokuwa Makamu wa Rais mwaka 2017, akishiriki kuchoma nyavu za uvuvi haramu kwenye Dampo la Buhongwa, wilayani Nyamagana, mkoani Mwanza. **PICHA: MTANDAO**

**Na Jenifer Gilla**

HATUA ya serikali kupiga vita matumizi ya mabomu zimechangia kuwapo uvuvi mbadala, ikiwamo nyavu za plastiki, ambazo nazo zinaelezwa kuwa na madhara kwa ikolojia ya bahari

Baadhi ya madhara yake ni kupotea kwa baadhi ya viumbe bahari, wakiwamo kobe wanaokufa kwa kujeruhiwa katika harakati za kujiokoa, baada ya kunaswa na nyavu.

Uvuvi wa nyavu za plastiki ulishapigwa marufuku nchini chini ya Sheria ya Uvuvi Mwaka 2003 na adhabu zake zinajulikana ni faini isiyopungua Sh.200,000 na isiyozidi Sh.milioni 15,000,000 au jela miaka isiyopungua miwili na isiyozidi miaka 10.

Nipashe limebaini kwamba, kukithiri vitendo hivyo katika ukanda wa Pwani ikiwamo mwalo wa samaki wa Kunduchi, jijini Dar es Salaam, unakinzana na kazi kubwa ya serikali kunusuru baioanuai hiyo.

Mvuvi Ibrahimu Ng'eve, anasema nyavu hizo huletwa na wafanyabiashara kutoka nchi jirani na wanaowauzia wavuvi wa nchini.

"Kwenye nchi za wenzetu wameruhusu kutumia zile nyavu, lakini kwetu hapa sisi sheria hairuhusu, kwa sababu zina madhara makubwa sana kwa samaki," anasema Ng'eve.

Hilo linafafanuliwa na Ofisa Uvuvi wa Wilaya ya Kinondoni, Godfrey Mrosso, anayesema baadhi ya wavuvi wanazitengeneza kwa kutumia mishipi ya ndoano za kuvulia samaki, ingawa shughuli hiyo inatumia muda mrefu.

"Zile nyavu ni zile za mshipi ambazo wanatumia wale wanaotumia ndoano kujipatia samaki, lakini inawezekana wakawapo watu wanaonunua hizo nyavu halafu wakaenda kusuka nyavu za kuvulia samaki, japo kufuma nyavu ni kazi... wapo wanaoweza, ingawa wanafanya hivyo kwa kujificha," anasema .

Mvuvi, Sadiki Chale, anasema wavuvi wanapenda kutumia nyavu hizo, kutokana na uwezo wake wa kukaa kwenye maji muda mrefu bila ya kuharibika na kukamata samaki wengi, jambo ambalo nyavu za kawaida haziwezi kufanya.

"Wenzetu hao wanasumbuliwa na tamaa ya kupata samaki wengi na kusahau maisha ya baadaye, kwa sababu zile nyavu zinanasa samaki wengi hadi wenyewe wanashindwa kuwabeba wote. Wengine wanawaacha wanakufa, madhara yake mazalia ya samaki yanazidi kupungua" anasema Sadiki.

> **"Zile nyavu ni zile za mshipi ambazo wanatumia wale wanaotumia ndoano kujipatia samaki, lakini inawezekana wakawapo watu wanaonunua hizo nyavu halafu wakaenda kusuka nyavu za kuvulia samaki, japo kufuma nyavu ni kazi...**

Anaeleza kuwapo wavuvi wanaozipaka sumu nyavu hizo, ili samaki anayenasa asitoke na hata wale wanaonusurika kwa hatimaye wanakufa kutokana na sumu wanayokutana nayo, zao lake ni samaki wapo hatarini kupungua.

Ripoti iliyotolewa na Shirika la Uhifadhi wa Mazingira Duniani (WWF) mwaka 2022 inayoitwa 'Stop Ghost Gear', inaonyesha matumizi ya vifaa vya uvuvi hatari, yanadhuru kwa kiasi kikubwa viumbe bahari.

Ina ufafanuzi kwamba vifaa hivyo hudhuru asilimia 66 jamii ya viumbe bahari kwa aina ya saba au viumbe bahari, wakiwamo ndege na kasa wa baharini, wakisababishiwa vifo vya taratibu.

**SURA YA MADHARA**

Mtaaluma, Prof. Philip Bwathondi, anasema uvuvi wa kutumia nyavu za plastiki huchangia samaki wengi kufa bila sababu za msingi, kutokana nyavu zile kunasa samaki wengi kuzidi uwezo wa wavuvi.

Anasema, samaki wengi wananasa kwenye mtego wa nyavu kiurahisi zinapokuwa majini, kutokana na rangi yake kufanana na maji.

Mwanazuoni huyo anafafanua kwamba, huwa wana kawaida ya kuziacha nyavu katikati ya bahari, kwa kuhofia watakamatwa nazo.

"Wanapoziacha kwenye bahari, samaki wengi wananaswa na hivyo wanapokuja kesho yake, wanakuta samaki wengi wamenaswa na wengine wamekufa. Hivyo, wanawachukua kiasi wanachotaka na kuacha wengine wakiendelea kufa," anasema.

Lingine analolitaja ni kwamba, nyavu hizo zina matundu madogo yanayonasa hadi samaki wachanga, ambao hawajakomaa kwa ajili ya kuliwa, hivyo inaathiri vizazi vyao katika viumbe bahari.

"Ukienda huko katikati ya bahari kama kuna eneo ambalo nyavu hizo zimetelekezwa, utakuta mamia ya samaki wamekufa baada ya kunaswa," anasema.

Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa, FAO linakadiria uvuvi haramu usioripotiwa na usiodhibitiwa, husababisha kupotezwa tani milioni 11 hadi 26 za samaki kila mwaka, huku hasara za kiuchumi ni kati ya Dola za Marekani bilioni 10 hadi 23, sawa na Sh. trilioni 23.37 hadi Sh. trilioni 53.751.

**MAPAMBANO YALIVYO**

Ofisa Uvuvi Mrosso, anasema serikali kwa kushirikiana na viongozi wa mialo ya samaki, wanaendelea kuwasaka wavuvi wote wanaofanya kazi hiyo kinyume na sheria ya uvuvi na adhabu inatolewa kwa wakosaji wanaokamtwa na kuthibitika; faini au jela.

"Tuliwakamata wavuvi wanaotumia nyavu hizo kama mwaka mmoja au miwili iliyopita, baada ya hapo tukawapeleka polisi wakachukuliwa hatua za kisheria. Kwa hivi karibuni, hatujafanikiwa kuwakamata, lakini inawezekana wapo wanaofanya kwa siri na sisi hatutochoka kuwasaka," anasema

Pia, anasema huwa wanatoa elimu ya madhara ya uvuvi haramu kwa jamii, viumbe bahari, mazingira, akiamini inatoa mwamko wamekuwa wakitoa taarifa, pale wanapomnasa mvuvi mwenzao akifanya vitendo hivyo.

Msimamizi wa Mazingira ya Bahari na Fukwe, anayeshughulika na masuala ya takwimu Msasani, Justine Ndola, anasema huwa wanafanya doria za usiku na pindi wanapogundua dalili za vikundi vya wavuvi haramu, wanatoa taarifa kwa polisi majini, wanaofuatilia na ikibainika uhalifu wanawakamata.

Kamanda wa Polisi Kikosi cha Wanamaji Tanzania, Moshi Sokoro, anasema shida yao kubwa ni namna ya kuwakamata, kwa kuwa nyavu wanaziacha baharini.

"Hizo nyavu wamekuwa wakiziacha ndani ya bahari, kwa sababu zenyewe haziozi tofauti na nyavu za kawaida," anasema

Aidha Msimamizi Mazingira, Andola anataja changamoto nyingine inayowakabili ni kukosekana vifaa vya kuwafuatilia, ikiwamo vya usafiri.

"Tuliwahi kupanga doria ya kuwasaka tukawakamata wavuvi kama unaenda kwa Nyerere (Msasani), walipotuona wakakimbia, sisi tukachukua nyavu na mitumbwi yao tukazileta hapa ofisini, baadae tukawapigia watu kutoka Ofisi ya Ofisa Uvuvi Kinondoni, wakaja kuzichukua," anabainisha.

**NINI KIFANYIKIE**

Mvuvi Ibrahimu Ng'eve, anasema serikali inapaswa kujenga utamaduni wa kupitia kila mara maeneo kunakofanyika uvuvi, na kushirikiana na wavuvi kuwabaini watu hao, kwa sababu wanafahamika.

Mkurugenzi wa shirika la Aqua Farm Organisation (AFO) linalojishughulisha na usalama wa viumbe bahari, anasema kuna haja ya serikali kutoa elimu inayojitosheleza kwa wavuvi na madhara ya kutumia neti hizo.

"Kikubwa hawa wavuvi bado elimu haijawaingia vizuri, kwa sababu mpaka sasa hawaelewi kuwa ule uvuvi una athari kubwa kwa uchumi wao hapo baadaye, serikali iwaeleze hili na ninaamini watabadilika," anasema.

AFYA

# Ilivyo vita vya kukabili kasi HIV, dawa kulevya Mwanza

## • Dk. Kahemele aeleza undani, mhanga afunguka...

**Na Pendo Thomas,** Mwanza

NI simulizi inayoanika namna ya kuharibiana maisha, kuanzia mwenendo wa tabia, hadi kuwa mtumiaji dawa kulevya.

Kijana (jina tunalo) ni mhanga mwenye simulizi ya safari yake, alivyonasa hadi alivyochomoka, akinena alianza safari yake katika sura kwamba, baada ya kufariki baba yake akiwa na umri mdogo miaka 13, mwanafuzi wa darasa la sita, akawa anapenda sana kwenda kuangalia runinga usiku kwenye mabanda.

Ni kitendo ambacho hakukipendelea hata siku moja, mama yake akamchapa sana hadi akaamua kutoroka nyumbani, maeneo ya Mganza, Chato, kwenda mkoani Mwanza ambako dada yake alikuwa anaishi.

"Nilitafutiwa kazi za ndani na dada kwa rafiki yake kwa ahadi ya mshahara wa shilingi 8,000 ambako nilitumikishwa kazi nyingi, kwenye nyumba mbili na nilikaa miezi mitatu bila ya kupewa malipo, hali iliyosababisha niondoke na kurudi kwa dada ambaye alinifokea na nikaamua kuondoka.

Anasema, akaamua kuelekea visiwani, akipataja visiwa vya Yozu, Mchangani na Zilagula vilivyopo wilayani Ukerewe, ambako alikutana na marafiki wanaovuta bangi, sigara, kunywa pombe na ni wachezaji wa disko usiku.

Binti huyo anasema binafsi hakujua pa kuelekea, akaangukia kujiunga na vitendo hivyo na baada ya miezi sita alirudi jijini Mwanza.

"Nikiwa sehemu nilizokuwa naenda kununua bangi, nilipata mwanaume wa kuishi naye ambaye pasipo kujua tukiwa tunaendelea na uvutaji huo, kumbe alikuwa akinichanganyia bangi na dawa za kulevya akitaja aina ya Heroine, ambayo alijikuta akiingia kwenye uraibu wa matumizi ya dawa za kulevya," anasema.

Anaeleza lengo la mwanaume huyo ilikuwa kumuingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya, ili aweze kumtumikisha kufanya biashara ya ngono na akawa anafanya hivyo kila siku, akikutana na wanaume wengi, kisha anampelekea pesa mwanaume huyo.

"Ililazimika nijiuze asubuhi, mchana na jioni ili nipate pesa ya kuvuta na kumvutisha huyo kijana na ilifika hatua nikakosa mtu wa kuniinua, nikaanza kuruka mageti kuiba kwenye nyumba za watu, ili kupata pesa ya kununua dawa za kulevya," anasema.

Kijana huyo anaendelea: "Mwaka 2013 nilipata mtoto na mwanaume tofauti na niliye kuwa nikiishi naye, ambaye alifariki siku chache baada ya kujifungua, kwani kutokana na matumizi ya dawa za kulevya, nilikuwa sihudhurii kiliniki kupata huduma za afya."

Anaeleza kutumia dawa za kulevya na kutumikishwa kingono kwa miaka 10 kuanzia mwaka 2008 akiwa na umri miaka 14 hadi mwaka 2018, alipoacha kutumia dawa hizo, akaanza matibabu maalumu katika kituo husika kilichopo kwenye Hospitali ya Rufani Sekou Toure, jijini Mwanza.

"Kwa kweli dawa za kulevya zimenipotezea mwelekeo nikiwa na umri mdogo na nimeambukizwa virusi vya Ukimwi na homa ya ini, kutokana na mwenendo mbaya nilio kuwa nao," anatamka kwa kauli ya majuto.



Dawa za kulevya, katika sura tofauti. **PICHA: MTANDAO**

> “Hakuna haja ya kujificha tena, dawa zipo na zinatolewa bure. Hakuna sababu ya mtu kujificha nyumbani ukijua una maambukizi ya virusi vya Ukimwi wakati huduma na matibabu inapatikana.



Mtaalamu, Dk. John Kahemele. **PICHA: PENDO THOMAS.**

### WADAU KINGA

Godfrey Kirumbe, mkazi wa Nyegezi, jijini Mwanza, anakumbusha haja ya jamii kuwalinda vijana wasijiingize katika utumiaji dawa za kulevya, akisisitiza hoja inapaswa kutolewa kwa upana katika jamii, kuanzia ngazi za chini ya elimu, kuwawezesha watoto kukua wakiwa na uelewa sahihi wa namna ya kuepukana na matumizi hayo.

Anashauri serikali inapaswa kutafuta suluhisho la udhibiti dhidi ya kuingizwa nchini, pia uzalishaji wa dawa hizo kwa kuwachukulia hatua kali wote wanaobainika kujihusisha na biashara hiyo, hata kuangukia katika madhara mbalimbali ndani ya jamii inayoshindwa kutekeleza majukumu ya ujenzi wa taifa.

Dk. John Kahemele, ni Naibu Mkurugenzi Mkazi kutoka taasisi isiyo ya kiserikali ICAP, anaitambulisha kuwa ni mshiriki mradi unaopambana na madhila hayo ya Ukimwi na dawa za kulevya, kupitia mpango wa dharura unaoitwa 'Pepfar' kwa kushirikiana na serikali ya Tanzania.

Mkoani Mwanza, penye simulizi tajwa, wanatekeleza huduma ya tiba na matibabu kwa wanaoishi na virusi vya ukimwi, pia kusaidia mabinti rika balehe walio kwenye mazingira hatarashi ya kupata maambukizi ya magonjwa, kupitia kituo cha kusaidia waraibu wa dawa za kulevya.

Anafafanua kwamba, Mwanza inakadiriwa kuwa na takribani watu 145,000 wanaoishi na maambukizi ya virusi vya Ukimwi na hadi Desemba 2022, wamefanikiwa kuwafikia watu 121,000 wakiamini ni hatua nzuri katika udhibiti wa maambukizi mapya na vifo kufikia sifuri ifikapo mwaka 2030.

Anatoa wito kwa wote wenye tatizo la uraibu wa dawa za kulevya, kuepukana na hali hiyo huku akiwaasa wasichana wadogo wanaojiingiza kwenye biashara ya ngono, kwamba wanapata mbadala wa kujifunza ujuzi mbalimbali unaowapa mwelekeo wa maisha, wakajitegemee.

"Hakuna haja ya kujificha tena, dawa zipo na zinatolewa bure. Hakuna sababu ya mtu kujificha nyumbani ukijua una maambukizi ya virusi vya Ukimwi wakati huduma na matibabu inapatikana," anatamka Dk. Kahemele.

Hapo, Mkuu wa Kitengo cha Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Ukimwi, katika mradi huo, Eveline Maziku, anasema wanaendelea kuyafikia makundi mbalimbali yaliyo hatarini kupata maambukizi hayo, wakiwamo watumiaji wa dawa za kulevya na wanaofanya biashara za ngono na washiriki wa mapenzi ya jinsia moja.

Anaeleza watumiaji dawa za kulevya wako hatarini zaidi, virusi vya Ukimwi na homa ya ini, kwani wamekuwa wakichangia vitu vyenye ncha kali pasipo tahadhari, huku wakijiingiza kwenye ngono zembe.

Pia, anaeleza serikali inaendelea kufanya jitihada za kutoa elimu kwa makundi hayo, ikijumuisha kuanzisha vituo vya tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya, ambao wamekuwa wakijengewa uwezo wa stadi za maisha, ili wajitegemee na kuepukana na uwezekano wa kurejea katika matumizi ya dawa hizo.



# TADB yazindua programu utoaji mikopo wanawake, vijana

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imezindua programu maalum ya mikopo ya kilimo kwa wanawake na vijana.

Mikopo hiyo imelenga kukabiliana na kero za mitaji kwa kundi hilo, kwa kulegeza baadhi ya vigezo na masharti ya mikopo ikiwamo kupunguza riba hadi asilimia nane.

Programu hiyo imezinduliwa juzi jijini Dodoma na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Akson, huku benki hiyo ikitoa Sh. milioni 50 kama mtaji wezeshi kwa makundi 100 ya wanawake na vijana ambapo fedha hizo zitawanufaisha watu 1,000 wanaoratibiwa chini ya Taasisi ya Tulia Trust.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Dk. Tulia aliipongeza TADB kwa kuanzisha programu hiyo ambayo itakuwa mwarobaini wa kero wanazopitia wanawake na vijana katika upatikanaji wa mitaji kwenye sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Dk. Tulia alitoa rai kwa wanawake na vijana kuchangamkia fursa hiyo adimu pamoja na kuwa wabunifu katika mazingira yanayowazunguka ili kujikwamua kiuchumi.

"Wanawake na vijana mnapaswa kuchangamkia fursa hiyo ili kuweza kujiinua kiuchumi katika kilimo na biashara mbalimbali mnazofanya," alisema Dk. Tulia.

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Frank Nyabundege, alisema benki hiyo itatoa mikopo ya hadi Sh. milioni 150 kwa mtu mmoja, huku ikitarajia kutoa Sh. milioni 500 kwa vikundi na taasisi zinazoundwa na makundi.

Hata hivyo alisema utekelezaji wa mikopo hiyo utaanza na kuwakopesha vijana wanufaika wa miradi na programu mbalimbali za vijana na wanawake ikiwamo na programu ya Building for Better Tomorrow (BBT).

Nyabundege alisema kupitia programu hiyo, TADB haiishii kutoa mikopo yenye riba nafuu peke yake, bali huduma za mikopo zilizolegezwa masharti zitaambatana na msaada usio wa kifedha, kama vile mafunzo, ushauri wa kibiashara na kuwaunganisha wazalishaji na masoko ya ndani na nje.

Wakati huo huo, kama ishara ya uzinduzi wa programu hiyo maalum, TADB ilitoa Sh. milioni 50, kama mtaji wezeshi kwa makundi 100 ya wanawake na vijana itakayowezesha wanufaika 1,000 wanaoratibiwa chini ya Taasisi ya Tulia Trust.

Alisema fedha hizo zitatolewa kwa riba ya asilimia sifuri na zitatumika kama mfuko wa mtaji unaojizungusha kwa makundi hayo ili fedha hizi ziendelee kuwanufaisha wakulima wengi zaidi.

Alisema benki hiyo inatarajia kutoa mikopo ya Sh. bilioni nane kwa wanawake na vijana zaidi ya 25,000 kwa ajili ya kujiinua kiuchumi.

Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika ya Mashariki na Kusini wa Kituo cha Kimataifa cha Utafiti wa Mboga na Matunda, Dk. Gabriel Rugalema alisema kituo hicho kitaendelea kushirikiana na Taasisi ya Tulia Trust pamoja na TADB kwa ajili ya kutoa mbegu mbalimbali za mboga ili kuzidi kuimarisha sekta ya kilimo hapa nchini.

# EIB kutoa tril.1.3/- kuwawezesha wanawake kwenye biashara

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BENKI ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya (EIB) kwa kushirikiana na serikali inatarajia kutoa mkopo wa Shilingi trilioni 1.3 kusaidia wanawake kuboresha biashara na uwekezaji kwenye mnyororo wa thamani katika sekta za mifugo na uvuvi.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Daniel Mushi, alibainisha hayo juzi wakati wa kikao cha wadau juu ya uwezeshwaji wa miradi ya uwekezaji kwenye mifugo na uvuvi kupitia dirisha la uwezeshwaji wa EIB kilichofanyika jijini hapo.

Dk. Mushi alisema dhumuni la fedha hizo ni kuwezesha sekta binafsi kuwa kichocheo cha maendeleo.

"Kwa kuanzia walengwa mahsusi ni sekta binafsi hususani kwa biashara zinazoongozwa na wanawake au shughuli zinazoambatana na uchumi wa buluu ikiwamo kilimo cha mwani,"alisema Dk. Mushi.

Aidha, Dk. Mushi alisema siyo tu kuwainua wanawake katika uwekezaji bali hata kuzalisha fursa za ajira kwenye mnyororo wa thamani wa mazao ya bahari na mifugo kwa ujumla na kupunguza ukosefu wa ajira nchini.

"Wajasiriamali watumie fursa hii vizuri ili iwe kioo na baadaye tuaminike ili fedha zijazo zipitie moja kwa moja kwenye sekta binafsi na fursa hii itakuja tena ikiwa tutakuwa waaminifu kwa kutumia vizuri mikopo hiyo,"alisema Dk. Mushi.

Mchumi kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Vidah Malle, alisema kuwa mkopo huo ni fursa pekee kwa sekta binafsi kukuza uaminifu kwa kutoa matokeo chanya ya fedha watakazozichukua.

"Sina uhakika kama fursa kama hii imewahi kupitia katika sekta binafsi mara nyingi hupitia taasisi za serikali. Kwa hiyo hii ni hatua nzuri na tumeoneshwa kuaminiwa, hivyo tujitahidi tutakapopata fedha hizo basi tulete matokeo chanya,"alisema Vidah.

Kaimu Mkuu kutoka Kitengo cha Kilimo Rejareja Benki ya NMB, Wogofya Mfalamagole, alisema wamejipanga kutoa mikopo hiyo kwa wawekezaji wote kwenye sekta binafsi kwa mujibu wa taratibu walizopangiwa na serikali kwa riba isiyozidi asilimia 10.

Mwekezaji na Katibu wa Chama cha Usindikaji wa Maziwa Tanzania (TAMPA), Rose Lyimo, alisema katika jamii kuna wanawake wengi wanaofanya shughuli za uwekezaji na hawana mitaji ya kutosha kupanua biashara, hivyo fedha hiyo itawasaidia kuwainua na kuonyesha uwezo wao.

Mkopo huo ambao unatajwa kuwalenga zaidi wanawake utakwenda moja kwa moja kwa sekta binafsi kupitia Benki za NMB, CRDB na KCB.



Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Dk. Sophia Kizigo (kushoto), akizungumza na wadau wa maendeleo pamoja na baadhi ya wakuu wa idara za wilayani humo, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mil.15/- zilizotengwa kwa ajili ya mkopo zakosa walengwa

**Na Ibrahim Joseph,** MPWAPWA

SHILINGI milioni 15 zilizotengwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mpwawa mkoani Dodoma kwa ajili ya mikopo ya asilimia 10 kwa makundi ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu zimekosa wakopaji.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Mpwapwa, Baraka Msuya, alibainisha hayo juzi alipokuwa akitoa taarifa wakati wa hafla ya kukabidhi hundi kwa vikundi vilivyoomba mikopo ya halmashauri hiyo.

Msuya alisema Sh. milioni 15 zilizotengwa kwa ajili ya mikopo ya watu wenye ulemavu kwenye halmashauri zimekosa watu wa kuchukua mikopo hiyo ambayo ni sehemu ya asilimia 10 ya mapato yao. Alisema halmashauri hiyo ilitenga Sh. milioni 18 kwa ajili ya kundi hilo la watu wenye ulemavu lakini waliojitokeza kuchukua mikopo ni watu wawili ambao wamechukua Sh. milioni tatu.

Aidha, alisema uhamasishaji unaendelea ili kupata waombaji watakaokopeshwa fedha hizo kulingana na maombi yatakayopokelewa kupitia mfumo wa usimamizi na utoaji wa mikopo ya asilimia 10.

Kadhalika alisema kuanzia Julai 2022 hadi Februari 2023 halmashauri hiyo ilitenga Sh. milioni 90 kwa ajili ya kukopesha makundi ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Alisema kati ya fedha hizo Sh. milioni 75 sawa na asilimia 83.3 ya lengo zimetolewa na kukopeshwa kwa vikundi vya vijana na wanawake pamoja na wenye ulemavu wawili.

Alifafanua kuwa vikundi vya wanawake saba vyenye idadi ya watu 43 vilikopeshwa Sh. milioni 36 na Sh.milioni 36 zingine zimekopeshwa kupitia kundi la vijana 30.

Msuya alisema vikundi vya wanawake vinaongoza katika kurejesha mikopo waliyokopa tofauti na vikundi vingine vya wakopaji.

Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Dk. Sophia Kizigo, akizungumza wakati wa kukabidhi hundi hiyo alitaka kiwango cha mikopo kuongezwa ili kuwasaidia wakopaji kuwa na mitaji mikubwa.

Dk. Kizigo alisema kiasi kinachotolewa kwa sasa hakitoshi kutokana na vikundi vya wakopaji kuwa vingi na idadi ya watu kwenye kikundi kimoja, hivyo wakichukua Sh.milioni tano ni fedha ndogo.

Hivyo, aliwataka wakopaji kulipa fedha za mikopo kutokana na biashara walioombea halmashauri na siyo kuchukua sehemu nyingine.

Alisema kuchukua fedha ya marejesho nje ya mapato ya mradi uliomba mkopo ni uharibifu wa bajeti ya familia.

Hata hivyo, aliwataka wakopaji kuomba msaada wa elimu ya biashara kutoka kwa maofisa wa halmashauri au taasisi za kifedha kabla ya kukopa ili kuepuka kupata hasara.



# Bil.20/- zatumika ujenzi hospitali, vituo vya afya, zahanati

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imetumia Sh. bilioni 20 kukamilisha miradi ya ujenzi wa hospitali mbili za wilaya, vituo vya afya 21, zahanati 23 pamoja na nyumba za watumishi.

Haya yalisemwa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, wakati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwenye maadhimisho ya miaka miwili ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema serikali imetekeleza ujenzi wa wodi ya wazazi yenye uwezo wa kuchukua vitanda 222 kwa ajili ya kulaza wagonjwa ujenzi ambao umegharimu Sh. bilioni 17 na kwamba vifaa vyote vimewasili.

"Pamoja na kulaza wagonjwa jengo hili limekuwa kama kivutio cha utalii, watu wanatumia kupiga picha mbalimbali za sherehe na limejengwa kwa namna ambayo wanaume wanaweza kuwepo na kushuhudia wakati wake zao wanajifungua,"alisema Homera.

Aliwashauri wanaume mkoani humo kuongozana na wake zao wakati wa kwenda kujifungua na kwamba kitendo cha kuwashuhudia wakijifungua kitawahamasisha wanaume wengi kuwajali wake zao. Alisema pia wamepokea mashine tatu za mionzi kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ya Mbarali na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya pamoja na Jiji zenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni moja.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Kanda ya Rufani Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji, alisema serikali kwa kushirikiana na Taasisi ya Saratani Ocean Road imetoa zaidi ya Sh. bilioni 50 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya utoaji matibabu kwa wagonjwa wa saratani.

"Tumekuwa na tatizo kwa wagonjwa wa saratani kusafiri kwenda Taasisi ya Saratani Ocean Road kwa ajili ya matibabu ya mionzi na huduma nyingine lakini hivi karibuni tuna mradi wa Sh. bilioni 50, tunaanza kujenga hospitali ya matibabu ya saratani katika Jiji letu la Mbeya," alisema Dk. Mbwanji.

Alisema mbali na ujenzi wa hospitali hiyo wanatarajia kufunga mashine ya kisasa kwa ajili ya kipimo cha MRI yenye thamani ya Sh. bilioni tatu ili kuwaondolea adha wagonjwa ambao wamekuwa wakifuata kipimo hicho katika mikoa ya Dodoma na Dar es Salaam.




Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akizungumza wakati wa uzinduzi wa programu maalum ya mikopo ya kilimo kwa wanawake na vijana jijini Dodoma jana. Kupitia mpango huo, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), imetenga Sh. bilioni 8 kwa ajili ya kuwakopesha wanawake na vijana 25,000 Bara na Zanzibar kwa riba nafuu ya asilimia 8. Wa pili kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Frank Nyabundege. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wananchi walia kupanda gharama gesi ya kupikia

**Na Grare Mwakalinga**, MBEYA

WANANCHI mkoani Mbeya wameiomba serikali kupunguza gharama za upatikanaji wa gesi safi kutokana na wananchi wengi kushindwa kumudu gharama.

Wakizungumza na Nipashe, mmoja wa wananchi hao, Triphonia Kabende, kutoka Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, (MUST) alisema pamoja serikali kuhamasisha wananchi kutumia nishati mbadala kwa lengo la kutunza mazingira jitihada hizo zinapaswa kwenda sambamba na kupunguza gharama kubwa za upatikanaji wa gesi nchini, ili kuwafikia wananchi wa kipato cha chini.

"Tumesikia serikali inakuja na mpango wa matumizi ya mabomba ya gesi lakini hadi sasa wananchi hawajui itakuaje ukilinganisha na ile ya kuweka kwenye mitungi, nashauri elimu itolewe lakini waangalie na gharama zake kwa wananchi kwa sababu gesi inauzwa kwa gharama ambayo wananchi wengi wa kipato cha chini hawawezi kumudu,"alisema Trifonia.

Benard Mwakasitu alisema kumekuwapo na uharibifu mkubwa wa mazingira kutokana na matumizi ya nishati isiyo safi hasa kuni na mkaa ambazo matokeo yake ni ukataji miti, hivyo serikali inapaswa kuweka mikakati itakayowezesha upatikanaji wa nishati mbadala kwa bei nafuu ili wananchi waachane na matumizi ya nishati zinazoharibu mazingira.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ushindani (FCC), Zaytun Kikula, alisema vikwazo wanavyokabiliana navyo watumiaji wa nishati safi ni gharama kubwa za upatikanaji wa nishati hizo ambapo wananchi wengi hawawezi kumudu gharama hizo.

# NGOs zatakiwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za vibali

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imeyataka mashirika yasiyo ya kiserikali kuendesha shughuli zao kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za vibali walivyopewa ili kuepuka mgongano wa kiutendaji ambao umekuwa ukijitokeza kwa baadhi ya mashirika.

Rai hiyo ilitolewa na Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Mbeya, Emmanuel Kilundo, wakati wa mafunzo ya kuwajengeza uwezo mashirika zaidi ya 60 yasiyo ya kiserikali mkoani Mbeya.

Kilundo alisema mashirika mengi yamekuwa yakiomba usajili kwa ajili ya kutekeleza shughuli fulani za kijamii lakini wanapohitaji fedha hujikuta wakikiuka sheria na miongozo waliyopewa wakati wa usajili.

"Mashirika yanapata fedha kwa kuandika maandiko, mfano alisajili kuhudumia watoto yatima lakini anaona tangazo limetolewa wanawezesha masuala ya kidemokrasia anaandika andiko akipata fedha anajikuta anatekeleza kitu ambacho hajapewa kibali na mwisho inaleta mgongano na wengine wanaofanya jambo kama hilo,"alisema Kilundo.

Aidha, alisema mashirika mengi yamekuwa hayawasilishi taarifa zao kila baada ya miezi mitatu kutokana na wengi kupuuza sheria na miongozo iliyowekwa na wengine kwa kisingizio cha kuwa hawakutekeleza kazi zao.

Ofisa Mwandamizi kutoka Shirika la FCS, Nicholaus Mhozya, alisema wanawajengea uwezo mashirika hayo kutokana na baadhi ya mapungufu ambayo wameyabaini katika uendeshaji wa mashirika ikiwamo uelewa mdogo wa sheria na miongozo ya ulipaji kodi inayosimamia mashirika hayo.

"Tunataka kuimarisha mahusiano mazuri kati yetu sisi, mashirika na serikali kwa sababu tukienda nje ya sheria tunaweza kujikuta tunapata adhabu ikiwamo kufutiwa usajili kwa hiyo tunataka tuzifahamu hizo sheria ili tuzifuate na hatimaye kazi zetu za kuhudumia jamii tuzifanye bila vikwazo," alisema Mhozya.

Elisha Kawago mmoja wa washiriki katika mafunzo hayo alisema vikwazo wanavyokutana navyo ni ukosefu wa fedha za ufadhili kwa ajili ya kuendeshea shughuli zao hali inayoleta changamoto katika ulipaji wa kodi.

"Mashirika mengi yamekuwa hayalipi kodi wala kutoa taarifa za fedha kwa sababu mashirika yanatofautiana kuna mengine hayana ufadhili yanajichanga yenyewe, hivyo wanashindwa kulipa kodi lakini yapo mengine yanapuuza tu,"alisema Kawago.

Elisha aliongeza kuwa mashirika mengi hayawasilishi taarifa zao za utendaji kutokana na wengi kuwa na uelewa mdogo wa masuala ya kisheria na miongozo ya mashirika na kuiomba serikali kuwa na mafunzo ya mara kwa mara kwa mashirika hayo ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mshiriki mwingine, Agnes Kiswaga alisema mashirika mengi yakishapata fedha hujisahau na kuanza kuendesha shughuli zao pasipo kufuata sheria na miongozo waliyopewa hali inayosababisha baadhi yao kufutiwa usajili.





# 'Athari mabadiliko tabianchi, uchafuzi wa mazingira ni janga la kidunia'

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, amesema athari zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi na uchafuzi wa mazingira ni janga la kidunia.

Amesema serikali inapaswa kuchukua hatua za haraka kuhimili mabadiliko hayo.

Aliyasema hayo juzi eneo la Bumbwini Kaskazini 'B' Unguja na Dunga Wilaya ya Kati Unguja, wakati akizungumza na viongozi wa mikoa, wilaya, halmashauri, mabaraza ya miji, masheha na watendaji kuhusu mpango wa serikali wa kurithisha Zanzibar kuwa ya kijani.

Alisema kutokana na athari hizo hivi sasa sehemu kadhaa za Zanzibar zinaendelea kuathirika kwa maji ya chumvi kuingia katika mashamba ya wakulima na mingine kukimbilia sehemu za makazi ya watu, huku kukiwapo mmong'onyoko mkubwa wa fukwe.

Othman alisema kutokana na hali hiyo, serikali inampango jumuishi wa kuirejesha Zanzibar kuwa ya kijani kwa kuwashajiisha wananchi kujenga utamaduni kupanda miti na kuitunza.

Alisema katika mpango huo serikali kwa kushirikiana na wananchi pamoja na vyombo vingine duniani itahimiza na kuhamasisha upandaji wa miti ya mikoko pamoja na ya matunda katika maeneo ya fukwe.

Alifahamisha kwamba Zanzibar inaendelea kupungukiwa na kiwango cha miti hasa ya asili na ya matunda kutokana na jamii kutokutilia maana utunzaji wa miti, licha kwamba miti ni uchumi na biashara lakini wanaendelea kuikata.

Aidha alisema tathmini ya mazingira duniani inaonyesha kuwapo na mabadiliko makubwa ya ongezeko la joto katika nchi zilizokuwa na baridi, huku baadhi ya nchi zenye baridi hali hiyo ikiongezeka maradufu jambo ambalo linaleta athari kubwa hasa kwa nchi maskini ikiwamo Zanzibar.

Othman alisema Zanzibar pia inakabiliwa na tishio la ukame na kuchangia uhaba mkubwa wa rasilimali ya maji katika ardhi, hivyo maji kulazimika kupatikana kupitia visima vya kina kirefu.

Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja, Sadifa Juma Khamis, alisema kwamba wilaya yake inakabiliwa na changamoto kubwa ya migogoro ya ardhi pamoja na uchimbaji wa mchanga holela jambo ambalo limechangia uharibifu wa mazingira katika wilaya hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini B Unguja, Hamid Seif Said, aliitaka jamii kuacha muhali kwa kuwatetea wahalifu na kuonya kwamba wilaya yake itaendelea kuwa na mikakati ya kukabiliana na tatizo la uchimbaji mchanga holela kwa mujibu wa sheria.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadidi Rashid, alisema kwamba licha ya mikakati iliyowekwa na serikali za mikoa na wilaya, lakini maeneo ya Kijiji cha Uzi Ngambwa na Bungi yapo hatarini kuathirika kutokana na kuwapo kasi ya uchimbaji mchanga.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akipokea tuzo maalum ya kuthamini mchango wake katika kupambana na UVIKO-19, kutoka kwa Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili (MUHAS), Dk. Harrison Mwakyembe, jijini Dar es Salaam juzi, wakati wa hafla ya ufunguzi wa Kongamano la Matokeo ya Tafiti za UVIKO -19 zilizofanywa na chuo hicho. **PICHA: IKULU**

# Waziri aagiza umiliki wa ardhi kurejeshwa serikalini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Rahma Kassim Ali, ameuagiza uongozi wa Kamisheni ya Ardhi Zanzibar na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Magharibi "B" Unguja kurudisha umiliki wa ardhi serikalini eneo la kilimo liliopo Kijiji cha Fujoni, kufuatia kutumika kinyume na utaratibu.

Alitoa agizo hilo juzi alipofanya ziara kutembelea eneo hilo baada ya kupata taarifa kutoka kwa mwananchi kuhusiana na uuzwaji wa eneo hilo.

Ardhi hiyo inayomilikiwa na Faki Rashed Faki lakini anadaiwa kukata viwanja na kuviuza kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kinyume na matumizi ya shughuli za kilimo yaliyowekwa na serikali.

"Hatua ya kurudisha serikalini eneo hii itakuwa ni funzo kwa wale wote ambao walipewa kwa ajili kuyaendeleza kwa shughuli za kilimo na badala yake kuyatumia kwa viwanja na kuuza," alisema Rahma.

Aidha, alisema Wizara ya Ardhi itahakikisha inafuatilia kwa makini maeneo yote ya ardhi yaliotengwa kwa kilimo na yeyote atakayegundulikana anakwenda kinyume na matumizi sahihi ya eneo hilo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Hata hivyo aliwataka wananchi wanapotaka kununua maeneo kufika Kamisheni ya Ardhi Zanzibar kwa sababu taasisi hiyo imeundwa kisheria katika kusimamia masuala yote yanahusiana na ardhi na umiliki.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuepusha migogoro ya ardhi inayoweza kuepukika endapo wananchi watafuata sheria.

Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini " B" Unguja, Hamidi Seif Said, ameahidi kulitekekeza agizo hilo na kusema hatosita kumchukulia hatua mtu yeyote atakayekwenda kinyume na maagizo ya serikali katika matumizi ya ardhi ya kilimo kwa maslahi ya nchi na taifa kwa ujumla.

Naye Faki Rashed Faki ambaye anadai kuwa eneo hilo la ardhi amerithi kutoka kwa mzazi wake hakujua kuwa ardhi iliyotengwa na serikali kwa ajili ya kilimo na kukabidhiwa wananchi hazitakiwi kuuzwa.

# Wanawake watakiwa kuanza mapema mchakato wa kugombea uchaguzi mkuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, amewataka wanawake wenye ndoto za kugombea na kushika nafasi za uongozi kuanza harakati mapema za kujiandaa ili kujihakikishia ushindi katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Alisema hali hiyo itasaidia kuwa na uwakilishi kutoka katika vyombo vya kutunga sheria na kutoa maamuzi pamoja na kushika nafasi za juu kwenye vyama vya siasa.

Aliyasema hayo jana Zanzibar wakati akizungumza na wanawake kutoka vyama mbalimbali vya siasa visiwani Zanzibar walioanza mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kugombea na kushika nafasi za uongozi.

Alisema kwa muda mrefu wanawake wengi wanashindwa kutimiza malengo yao licha ya kuwa na nia ya kuwa viongozi na utafiti unaonyesha kuwa miongoni mwa sababu zinazosababisha ni kutojiandaa mapema.

Pia, aliwataka wanawake na washiriki wa mafunzo hayo kutokata tamaa licha ya matatizo mbalimbali watakazozipitia zikiwamo za kukatishwa tamaa kwa makusudi na watu wenye dhamira mbaya dhidi yao.

Dk. Mzuri pia aliitaka serikali kupitia Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi, kuhakikisha wanafuatilia kwa umakini suala la rushwa katika uongozi ili kuwabaini na kuwachukulia hatua stahiki wote wanaojihusha na vitendo hivyo.

Hata hivyo alisema uwepo madarakani kwa Rais Samia Suluhu Hassan ni kielelezo tosha kinachoonyesha uwezo wa kiongozi mwanamke ambacho wanawake wa Zanzibar wanapaswa kukitumia kama sehemu ya kusonga mbele.

Mkufunzi wa mafunzo hayo, Dk. Salum Suleiman Ali, kutoka Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) alisema wanawake wa Zanzibar wanauwezo mzuri wa kuwa viongozi, hivyo ni vyema kujiamini na kujiandaa.

Alisema wanawake lazima wajitambue na kujiwekea malengo tangu awali na kuwa na utaratibu wa kujiandaa katika kila hatua kwenye mchakato wake. Aidha alisema wanawake wanapaswa kuacha hofu na kujitoa katika midahalo mbalimbali ambayo inamjenga mwanamke katika kutambua upangiliaji wa hoja ambazo zitamwezesha kukubalika kwa haraka zaidi kwenye jamii.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na TAMWA-Zanzibar kupitia mradi wa kuwawezesha wanawake katika uongozi unaofadhiliwa na Ubalozi wa Norway.

# MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**PROSPER FRIDOLIN HENJEWELE** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba AB427948 iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 24/08/2010. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu naye au Ofisi ya Uhamiaji. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/4132/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MARY P. MCHOMVU** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba: **S2033-0057** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **VIWANDANI SECONDARY SCHOOL** mwaka **2009.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: MTW/NEW/RB/55655/2023**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya yaSINGIDA**
**Kituo cha UTEMINI Mkoa SINGIDA**
**Shauri la madai/Ndoa Na 30/2023**
**Jina la mdai ABASI ALLY KHAMA**
**Jina la Mdaiwa AMINA BAKARI NG'OMBO**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za mwanzo)**
**Kwa AMINA BAKARI NG'OMBO**
**Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba(eleza hapa habari za madai)**

**MADAI YA TALAKA, CHUMO LA PAMOJA NA MATUNZO YA MTOTO**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 24 mwezi 03 mwaka 2023 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.
**ANGALIZO**
Kama hautohudhuriasiku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa mahakama hii leo tarehe 24 mwezi wa 03 mwaka 2023

24/03/2023
HAKIMU
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
UTEMINI

---

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MOSHI DISTRICT REGISTRY**
**AT MOSHI**
**CIVIL CASE NO. 15 OF 2022**
**CRDB BANK PLC............PLAINTIFF**
**VERSUS**
**KILIMANJARO SAR LIMITED ............1ST REPONDENT**
**AMOUR ALLY ABDALLAH..............2ND RESPONDENT**
**IVAN BRAUN..............3RD RESPONDENT**

**TO: KILIMAJARO SAR LIMITED**
**NOTICE FOR MENTION**
**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention in the High Court of Tanzania at **Moshi on 29th march, 2023** at **9:00 a.m** before Honourable **J.L MASABO**, Judge.
**WHEREAS:** Service on you has been ordered to be published in the Nipashe Newspaper.
You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely upon in support of your case.
**TAKE FURTHER NOTE THAT:** In default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.
**GIVEN UNDER** my hand and seal of the court this **23rd day of February, 2023.**

DEPUTY REGISTRAR

---

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MOSHI DISTRICT REGISTRY**
**AT MOSHI**
**CIVIL CASE NO. 15 OF 2022**
**CRDB BANK PLC............PLAINTIFF**
**VERSUS**
**KILIMANJARO SAR LIMITED .........1ST REPONDENT**
**AMOUR ALLY ABDALLAH............2ND RESPONDENT**
**IVAN BRAUN............3RD RESPONDENT**

**TO: IVAN BRAUN**
**NOTICE FOR MENTION**
**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention in the High Court of Tanzania at **Moshi on 29th march, 2023** at **9:00 a.m** before Honourable **J.L MASABO,** Judge.
**WHEREAS:** Service on you has been ordered to be published in the Nipashe Newspaper.
You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely upon in support of your case.
**TAKE FURTHER NOTE THAT:** In default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.
**GIVEN UNDER** my hand and seal of the court this 23rd day of February, 2023.

DEPUTY REGISTRAR

---

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MOSHI DISTRICT REGISTRY**
**AT MOSHI**
**CIVIL CASE NO. 15 OF 2022**
**CRDB BANK PLC......PLAINTIFF**
**VERSUS**
**KILIMANJARO SAR LIMITED ......1ST REPONDENT**
**AMOUR ALLY ABDALLAH.........2ND RESPONDENT**
**IVAN BRAUN.........3RD RESPONDENT**

**TO: AMOUR ALLY ABDALLAH**
**NOTICE FOR MENTION**
**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention in the High Court of Tanzania at **Moshi on 29th march, 2023** at **9:00 a.m** before Honourable **J.L MASABO,** Judge.
**WHEREAS:** Service on you has been ordered to be published in the Nipashe Newspaper.
You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely upon in support of your case.
**TAKE FURTHER NOTE THAT:** In default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.
**GIVEN UNDER** my hand and seal of the court this 23rd day of February, 2023.

DEPUTY REGISTRAR

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AVTAR SINGH BASSAN**
anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 246 AQR – TOYOTA CALDINA.** Chassis No. **ST1910094270.** Engine **No. 3S177971.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/103467/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JOHN DAVID LAIZER**
anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 703 AFY.** Chassis No. **LMHPCJL7580101654.** Engine **No. 157FMI80101745.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/65463/2023.**

---

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**AT KIGOMA**
**(KIGOMA DISTRICT REGISTRY)**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 1 OF 2022**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE FR.RAYMOND KIPFUMU SABA .................DECEASED.**

**AND**

**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR THE LETTERS OF ADMINISTRATION**

**BY**

**FR. SABAS BANSHILAHE....................PETITIONER**

**GENERAL CITATION**

All person claiming to have any interest in the estate of the above –named deceased who died intestate, are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before granting of letters of administration is made to the above-named applicant.
Objections to the grant should be filed on or before the 19th day of April, 2023.
Dated 14/3/2023.

Deputy Registrar

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Kilolo.............KILOLO**

**Kituo cha KILOLO............................MKOA IRINGA**

**Shauri la madai No 01/2023**

**Jina la mdai MOHAMED AFRICA LTD.**

**Kwa RAYMOND PETRO NGUYA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**UNAAMULIWA NA MAHAKAMA KUJA KUJIBU KESI YA MADAI NO 01/2023 DHIDI YA MOHAMED AFRICA LTD.**
Tarehe 04 mwaka 2023 saa 8:30 asubuhi katika Mahakama Hii bila kukosa
Siku hiyo nisiku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi /mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea
Kama hautohudhuria siku hiyo na ikathibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo
Hati hii imetolewa leo tarehe 20 mwezi wa 03 mwaka 2023

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**AYUBU HUSSEIN KAMTI**
anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 289 CBX – SUZUKI CARRY.** Kadi ya gari yenye namba za usajili **T 292 CBX - SUZUKI CARRY.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/KIM/RB /104602/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**AYUBU HUSSEIN KAMTI**
anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 598 ANQ – NISSAN SUNNY.** Kadi ya gari yenye namba za usajili **T 288 CBX – SUZUKI CARRY.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/KIM/RB /104602/2023.**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF IRINGA**
**AT IRINGA**
**CIVIL CASE No. 8/2023**
**LAURENCE CHOMBO KYANDO .............PLAINTIFF**
**Versus**
**KIPONDOGORO AUCTION MART LTD..........1st DEFENDER**
**FINCA IRINGA....... ................2ND DEFENDANT**

**TO LAURENCE CHOMBO KYANDO**
**NOTICE OF DATE FOR MENTION**
The notice that the above case has been fixed for mention on 28 day of March 2023 at 08: a.m before Hon Z.A. Mpangule, Resident Magistrate
YOU ARE required appearing in this Court without fail and you must produce on that day all documents upon which you intend to rely in support your case

**GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 07 Day of March 2023**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SALIMU BAKARI MMBAGA**
anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 175 DJJ -** king lion Iliyotolewa na TRA. Taarifa imetolewa kituo cha polisi Arusha nakupewa kumbukumbu No. **ARU/MUR/RB/94974/2023**


***OFISI ZA MATANGAZO***
***Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.***
***Mobile: +255 - 745 700 710.***
***E-mail: advertise@guardian.co.tz,***
***Website: www.ippmedia.com***

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## UN: Kimbunga Freddy kimeathiri watu 500,000

**LILONGWE,** Malawi

UMOJA wa Mataifa (UN), umesema zaidi ya watu nusu milioni wameyahama makazi yao kutokana na kimbunga kikali Freddy na kuonya kuhusu kuongezeka kwa mahitaji ya kiutu.

Eneo la kusini mwa Malawi, lilikumbwa na mvua kubwa ya kiwango cha miezi sita ndani ya siku sita.

Mafuriko na maporomoko ya ardhi yalisomba nyumba, barabara na madaraja. Kimbunga hicho kilisababisha vifo vya karibu watu 500 kusini mwa nchi hiyo.

Wengine 150 walikufa katika nchi nyingine za kusini mwa Afrika, tangu mwishoni mwa Febrauri kwa mujibu wa takwimu za UN.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Uhamiaji (IOM), lilisema operesheni za utafutaji na uokozi zinaendelea.

IOM, ilisema zaidi ya watu 1,000 wamehamishiwa maeneo salama na zaidi ya makazi ya dharura 500 kufunguliwa nchini Malawi. **DW**

## Japan yaahidi msaada zaidi kwa Ukraine

**Tokyo,** JAPAN

WAZIRI Mkuu wa Japan, Fumio Kishida, amefanya ziara isiyotarajiwa mjini Kyiv kwa mazungumzo na Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, akiahidi msaada kwa nchi hiyo.

Zelensky alimtaja Kishida, kuwa mtetezi shupavu wa taratibu za kimataifa na rafiki wa muda mrefu wa Ukraine.

Naibu Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Ukraine, Emine Dzheppar, aliisifu ziara hiyo ya kihistoria akisema ni ishara ya ushirikiano wenye nguvu kati ya nchi hizo mbili.

Kishida, aliiahidi Ukraine msaada wa kifedha pamoja na wa kiutu na matibabu.

Waziri Mkuu huyo wa Japan alitarajiwa kurejea Tokyo baada ya ziara yake ya India, ingawa akaibadili mipango yake na kuzuru Ukraine.

Wakati wa ziara yake, Kishida alitembelea Bucha, mji wa mdogo karibu na Kyiv, ambako maofisa wa eneo hilo walisema, mamia ya miili ya raia ilipatikana.

Japan, imejiunga na washirika wa Magharibi katika kuiwekea vikwazo Russia, kwa uvamizi wake wa Ukraine.

Kishida, alikuwa ndiye kiongozi pekee wa kundi la nchi tajiri duniani, G7, ambaye hakuwa amezuru Ukraine, tangu Russia, ilipoanza uvamizi kamili nchini humo Februar, jana. DWIOM, ilisema zaidi ya watu 1,000 wamehamishiwa maeneo salama na zaidi ya makazi ya dharura 500 kufunguliwa nchini Malawi. **DW**



Rais Yoweri Museveni. **PICHA: MTANDAO**

# ‘Jela maisha wahusika mapenzi jinsia moja’

**Kampala,** UGANDA

MUSWADA umepitishwa na Bunge la Uganda ambao utatoa amri ya kisheria, watu wanaojitambulisha kuwa wapenzi wa jinsia moja, kuwa wahalifu.

Baada ya muswada hu mjadala umezuka maeneo tofauti duniani na hofu miongoni mwa jamii ya LGBTQ.

“Kuna ulaghai mwingi. Watu wanapokea simu ambazo usiponipa pesa, nitaripoti kwamba wewe unashiriki uhusiano wa jinsia moja,” mwanaharakati aliongea na chombo cha habari.

Watu binafsi wanaweza kukabiliwa na vifungo vya muda mrefu, ikiwa muswada huo utatiwa saini na Rais Yoweri Museveni kuwa sheria.

Uhusiano wa jinsia moja umeharamishwa katika nchi hiyo ya Afrika Mashariki. Ingawa, muswada wa kupinga mapenzi ya jinsia moja, unalenga kwenda mbali zaidi na kuwafanya watu kuwa wahalifu kwa msingi wa utambulisho wao wa kijinsia.

Ilipitishwa kwa uungwaji mkono mkubwa katika bunge la Uganda, juzi, jioni nchini humo.

Chini ya sheria iliyopendekezwa, marafiki, familia na wanajamii watakuwa na wajibu wa kuripoti watu walio katika mahusiano ya jinsia moja kwenye mamlaka.

“Katika baadhi ya maeneo hata wasimamizi wa sheria wanatumia mazingira ya sasa kuwanyang’anya fedha watu wanaowatuhumu kuwa wapenzi wa jinsia moja. Hata baadhi ya familia zinaripoti watoto wao polisi.”

**Katika baadhi ya maeneo hata wasimamizi wa sheria wanatumia mazingira ya sasa kuwanyang’anya fedha watu wanaowatuhumu kuwa wapenzi wa jinsia moja. Hata baadhi ya familia zinaripoti watoto wao polisi.**

Muswada huo, sasa utawasilishwa kwa Rais Museveni ambaye anaweza kuchagua kutumia kura yake ya turufu na kudumisha uhusiano mzuri na wafadhili na wawekezaji wa Magharibi au la, kwa kutia saini kuwa sheria.

Alitoa kauli kadhaa dhidi ya wapenzi wa jinsia moja katika wiki za hivi karibuni na pia alikosoa nchi za Magharibi kwa kuweka shinikizo kwa Uganda, juu ya suala hilo.

Mwanaharakati mwingine wa LGBTQ+ aliishutumu serikali kwa kutumia muswada huo, kuvuruga umma kutokana na kushindwa kwake kushughulikia baadhi ya matatizo yao ya kiuchumi.

“Wanajaribu kuibua masuala yakupinga wapenzi wa jinsia moja ili kugeuza mawazo kutoka kwa kile ambacho ni muhimu kwa Waganda kwa ujumla.

“Hakuna sababu kwa nini unapaswa kuwa na mswada unaoowafanya watu kuwa na hatia ya kuwa na mahusiano ya watu wazima wa jinsia moja,” Clare Byarugaba, Mwanaharakati wa Haki za LGBTQ+ Uganda, alisema.

Wanaounga mkono muswada huo walisema, wanajaribu kuwalinda watoto lakini Bi Byarugaba alisema: “Uwe unashiriki mapenzi ya jinsia moja au la, serikali na bunge wanapaswa kuanzisha sheria au angalau kutekeleza sheria zilizoko zinazolinda watoto wote.

“Wavulana, wasichana dhidi ya unajisi. Suala la kuwashirikisha watoto katika mahusiano ya jinsia moja halijathibitishwa, halina msingi, lina upendeleo.”

### MUSWADA WENYEWE

Toleo la mwisho bado halijachapishwa rasmi, ingawa vipengele vilivyojadiliwa bungeni ni pamoja na: Mtu anayepatikana na hatia ya kulea au kusafirisha watoto kwa madhumuni ya kuwashirikisha katika vitendo vya wapenzi wa jinsia moja anakabiliwa na kifungo cha maisha jela.

Kadhalika, watu binafsi au taasisi zinazounga mkono au kufadhili shughuli au mashirika ya haki za LGBT au kuchapisha, kutangaza na kusambaza nyenzo na fasihi za vyombo vya habari vinavyounga mkono wapenzi wa jinsia moja, pia watakabiliwa na mashtaka na kufungwa gerezani.

Pia kikundi cha wabunge wachache wa Uganda katika kamati inayochunguza muswada huo, hawakukubaliana na msingi wake. Wanasema makosa ambayo inataka kuharamisha tayari yamejumuishwa katika Sheria ya Kanuni ya Adhabu ya nchi.

Mwaka wa 2014, Mahakama ya Kikatiba ya Uganda, ilibatilisha kitendo kingine ambacho kilikuwa kimeimarisha sheria dhidi ya jumuiya ya LGBT.

Ilijumuisha kuifanya kuwa haramu kukuza na kufadhili vikundi na shughuli za LGBT na pia kusisitiza kwamba vitendo vya wapenzi wa jinsia moja, vinapaswa kuadhibiwa kwa kifungo cha maisha na ilishutumiwa sana na nchi za Magharibi.

Mahakama iliamua kwamba, sheria hiyo ibatilishwe kwa sababu ilipitishwa na bunge bila idadi ya wabunge inayotakiwa.

Mahusiano ya watu wa jinsia moja, yamepigwa marufuku katika nchi zipatazo 30 za Afrika na watu wengi wanashikilia maadili ya kihafidhinaya kidini na kijamii.

**BBC**

# CHAMA, KANOUTE WAIPANDISHA MZUKA SIMBA NUSU FAINALI CAF

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Simba umesema kitendo cha wachezaji wao wanne kutajwa kwenye kikosi bora cha wiki cha Ligi ya Mabingwa Afrika, ni tafsiri kubwa ya timu yao kuwa na wachezaji wazuri na wanaamini watawezesha kucheza nusu fainali ya michuano hiyo.

**Wachezaji wa Simba walioingia katika kikosi bora cha wiki cha Ligi ya Mabingwa ni Shomari Kapombe, Jean Baleke, Clatous Chama na Sadio Kanoute ikiwa ni baada ya kufanya vizuri na kusaidia Simba kufuzu hatua ya robo fainali.**

Mbali na kuingia kwenye kikosi bora cha wiki, Chama na Kanoute ni miongoni mwa wachezaji wanne wanaowania tuzo ya mchezaji bora wa wiki wa Ligi ya Mabingwa Afrika sambamba na Mahmoud Kahraba na Pecy kutoka Al Ahly.

Katika mchezo uliopita, Simba iliibuka na ushindi wa mabao 7-0 dhidi ya Horoya AC ya Guinea, mchezo ukipigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam huku Chama akitupia matatu (hat-trick) na Kanoute mawili, shukrani pia zikimwendea Jean Baleke aliyecheka na nyavu mara mbili.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kitendo cha wachezaji wao kuingia katika kikosi bora cha wingi na Chama na Kanoute kuwapo katika kinyang'anyiro cha tuzo ya mchezaji bora wa wiki kwenye Ligi ya Mabingwa, ni ishara kubwa kuwa Simba ina wachezaji bora.

Alisema wachezaji kufikia hatua hiyo si kitu cha kubahatisha na anaimani wakiongeza kujituma zaidi kwenye michezo iliyopo mbele yao watatinga nusu fainali.

"Unajua kitendo cha nyota wanne kuingia katika kikosi bora cha Ligi ya Mabingwa Afrika cha wiki, ilhali kuna wachezaji wengi walizitumikia timu zao huku Chama na Kanoute wakiingia katika kinyang'anyiro cha kuwania tuzo ya mchezo bora wa wiki, hiyo ni hatua kubwa.

"Hii ni ishara nzuri na inaonyesha tuna wachezaji wanauwezo mkubwa kama hao, wakiongeza nguvu kuhakikisha tunapambana katika hatua inayofuata basi nina imani Simba itacheza nusu fainali," alisema Ahme.

Aidha, Ahmed alisema baada ya mapumziko mafupi wachezaji wasiokuwapo katika majukumu ya timu za taifa wanaanza mazoezi kesho kujiandaa na mchezo wao dhidi ya Raja Casablanca.

Meneja habari huyo aliongeza kuwa watakuwa na mazoezi ya uwanjani na wachezaji kurudi majumbani kwao hadi hapo wachezaji wanaozitumikia timu zao za taifa watakaporejea na kuingia kambini kujiandaa na mechi yao ijayo.

Simba inatarajia kusafiri kuelekea nchini Morocco kukabiliana na wenyeji wao, Raja Casablanca katika mchezo wa kukamilisha ratiba ya hatua ya makundi utakaopigwa Machi 31, mwaka huu katika Uwanja wa Mohammed V, wenye uwezo wa kubeba mashabiki 67,000.

Simba yenye pointi tisa na Raja Casablanca alama 13, tayari zimefuzu kucheza hatua ya robo fainali kutoka Kundi C, hivyo mchezo wao utakuwa ni wakulinda heshima na kukamilisha ratiba tu, kwani hata kama Wekundu wa Msimbazi watashinda hawataweza kuwapiku Wamorocco hao na kuongoza kundi.




Wasanii wa Kikundi cha Ngoma za Asili cha Mwinuka Bendi, wakitumbuiza wakati wa mkutano wa kujadili kupambana na taka zitokanazo na vifaa vya umeme (electronics) pamoja na utunzaji wa mazingira kwa nchi za Afrika Mashariki ulioandaliwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, TCRA. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Coastal na mipango kujinasua 'play off'

**Na Hadija Mngwai**

TIMU ya Coastal Union ya jijini Tanga, imesema kwa sasa imeandaa mikakati madhubuti ya kuhakikisha inajikwamua katika nafasi ya hatari ya kucheza michezo ya mchujo (play off) kusaka nafasi ya kubaki Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Kwa mujibu wa kanuni za Ligi Kuu Bara, timu mbili zitakazoburuza mkia (ya 15 na 16), zitashuka moja kwa moja kwenda kucheza Ligi ya Championship msimu ujao, wakati zitakazomaliza nafasi ya 13 na 14, zitalazimika kucheza mechi za play off ili kuwania kubaki Ligi Kuu. Ligi Kuu Bara kwa sasa ipo ukingoni zikiwa timu zote zikibakiza michezo mitano kufikia mwisho wa msimu wa 2022/23, isipokuwa Simba na Yanga tu ambazo zimebakisha mechi sita kila mmoja.

Costal Union ipo katika nafasi ya 13 ikiwa na alama 26, ambayo ni ya kucheza michezo ya play off. Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Coastal Union, Jonathan Tito, alisema wanajipanga ipasavyo kuhakikisha wanafanikiwa kumaliza katika nafasi nzuri kwa kushinda michezo yote iliyobaki.

"Kikosi chetu kimeingia kambini leo 'jana' kikitokea mapumziko ya wiki moja baada ya mchezo wetu wa mwisho dhidi ya Singida Big Stars.

"Mchezo wetu unaofuata ni dhidi ya Dodoma Jiji ambao tutacheza katika Uwanja wa Jamhuri Dodoma, hivyo mwalimu anakiandaa vema kwa ajili ya ushindi," alisema Tito.

# Yanga yaivutia kasi Mazembe

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha wachezaji wa Yanga waliosalia nchini, kitaanza mazoezi leo Kigamboni jijini Dar es Salaam, tayari kwa maandalizi ya kuivaa TP Mazembe, mechi itakayopigwa Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Aprili 2, mwaka huu.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, amesema wachezaji wote wanatarajia kuripoti leo baada ya mapumziko ya siku tatu tangu Jumapili iliyopita ilipocheza dhidi ya US Monastir ya Tunisia na kushinda mabao 2-0, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na kukata tiketi ya kwenda robo fainali ya Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Hata hivyo alisema wachezaji watakaoripoti ni wale ambao hawakuitwa kuzitumikia timu zao za taifa, akibainisha kuwa kambi rasmi itaanza Jumatatu ijayo.

"Kesho wachezaji wote wataripoti kesho mazoezini baada ya siku tatu za mapumziko, kambi rasmi kwa ajili ya mechi ya TP Mazembe itaanza tarehe 27, Machi na kwa wachezaji wengine walio timu zao za taifa tutajumuika nao huko huko, lakini wapo wengine ambao tutaondoka nao hapa hapa nchini Machi 30," alisema Kamwe."

Ofisa Habari huyo amewataka wanachama na mashabiki wanaotaka kwenda kuishangilia timu hiyo kujitokeza kwani itakuwa ni kama sehemu ya mtoko na kushangilia mafanikio makubwa ya timu hiyo, baada ya kufanikiwa kutinga hatua hiyo.

Mechi hiyo itachezwa Uwanja wa TP Mazembe, ukiwa hauna umuhimu wowote zaidi ya matokeo yake kujulikana timu gani kati ya Yanga na US Monastir itaongoza kundi na itakayoshika nafasi ya pili, lakini zote mbili zikiwa zimefuzu hatua hiyo.

Mechi hiyo, pamoja na ya US Monastir itakayokuwa nyumbani dhidi ya Real Bamako ndiyo itakayoamua timu ipi itaongoza kundi hilo kwani kwa sasa zote zina pointi 10, Yanga ikiongoza kwa mabao ya kufunga baada ya kucheka na nyavu mara nane, Watunisia hao wakiwa na mabao sita.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema ni mechi muhimu na ngumu kwao hivyo, mapumziko mafupi ya siku mbili aliyowapa wachezaji ambao hawako katika majukumu ya timu zao za taifa yamemalizika na leo wanaendelea na mazoezi ya uwanjani kuanza maandalizi ya mechi iliyopo mbele yao.

Alisema wakati wachezaji waliopo katika majukumu ya timu zao za taifa wakiendelea na mazoezi na waliobaki wanatakiwa kuendelea na programu ya mazoezi kwa ajili ya kujiweka fiti ili watakapoungana wachezaji wote wanakuwa na hali sawa ya utimamu wa mwili.

"Baadhi ya wachezaji wetu wakiwa katika majukumu ya timu zao za taifa, waliobaki wanaendelea na programu ya mazoezi ya uwanjani kuwaweka fiti kwa sababu tuna mechi ngumu mbele ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya TP Mazembe," alisema Nabi.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### DISASI AWANIWA UNITED

KLABU ya Manchester United imeongeza nia ya kumnunua beki wa kati wa Monaco, Axel Disasi, 25. ***(Mail)***

### SHEIKH KUONGEZA MZIGO

SHEIKH Jassim bin Hamad Al-Thani yuko tayari kuongeza ombi lake la kuinunua Manchester United hadi pauni bilioni 5.5. ***(The Mirror)***

### NEVES ANYATIWA LIVER

MANCHESTER United na Liverpool zinaongoza mbio mbele ya Barcelona katika nia ya kumnunua kiungo wa kati wa Wolves na Ureno, Ruben Neves, 26. ***(Football Insider)***

### POCHETTINO ANUKIA SPURS

WACHEZAJI wa Tottenham Hotspur wamekuwa wakiwasiliana na kocha wa zamani, Mauricio Pochettino, kuhusu uwezekano wa kurejea katika klabu hiyo. ***(Sky Sports)***

### AUBAMEYANG KUREJEA BARCA

MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang, mwenye umri wa miaka 33, anaweza kurejea Barcelona kama chaguo la bei ya chini miezi 12 tu baada ya kuhamia Stamford Bridge. ***(Mundo Deportivo)***

### OSIMHEN ATAJWA PSG

PARIS Paris St-Germain ndio klabu ya hivi punde zaidi kufikiria kumnunua mshambuliaji wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen, 24. ***(Foot Mercato)***

### MODRIC MKATABA MPYA

REAL Madrid bado ipo kwenye mazungumzo na kiungo wa kati wa Croatia, Luka Modric, kuhusu mkataba mpya wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37, ambaye amezivutia Klabu za Saudi Arabia na Qatar. ***(Sky Sports)***

### SPURS KUMKOSA LENGLET

KLABU ya Tottenham Hotspur haina uwezekano wa kutumia chaguo la kumsajili kwa mkopo mlinzi wa kati wa Ufaransa, Clement Lenglet, mwenye umri wa miaka 27, kutoka Barcelona. ***(AS)***

### MILNER KUKATWA MSHAHARA

KIUNGO wa kati wa zamani wa England, James Milner, mwenye umri wa miaka 37, atalazimika kukatwa mshahara ili aweze kupewa mkataba mpya na Liverpool. ***(Football Insider)***

### WOLVES KUINUNUA OOSTENDE

WAMILIKI wa Wolves wako kwenye mazungumzo ya kununua hisa katika klabu ya Ubelgiji ya K.V. Oostende. ***(Guardian)***

### AUBA KUACHIWA CHELSEA

CHELSEA inaweza kumwachia Pierre-Emerick Aubameyang kutoka katika mkataba wake msimu huu wa majira ya joto. ***(Sport)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MASTAA BRAZIL WAMTAKA ANCELOTTI KUTUA KUINOA

**RIO DE JANEIRO,** Brazil

GOLIKIPA wa Manchester City, Ederson, anataka Real Madrid iondolewe kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya ili Kocha Carlo Ancelotti aende Brazil "haraka iwezekanavyo."

**Ancelotti yuko chini ya mkataba kule Madrid hadi mwishoni mwa msimu ujao na Shirikisho la Soka la Brazil hivi karibuni lilikanusha kuwa lilifikia makubaliano na Muitaliano huyo mwenye umri wa miaka 63.**

Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Brazil wanaonekana kujiamini kuwa Ancelotti anaweza kuwa kocha wao ajaye.

Limekuwa gumzo miongoni mwa kikosi kitakachoshiriki mechi ya kirafiki ya wikendi hii huko Morocco.

> ●●● Nilikuwa nikijadili hili na Casemiro, Vinicius Junior, (Eder) Militao, kuna uwezekano...

"Nilikuwa nikijadili hili na Casemiro, Vinicius Junior, (Eder) Militão. Kuna uwezekano mkubwa kwamba atakuja," alisema Ederson katika mkutano na waandishi wa habari Jumanne.

Kazi hiyo imekuwa wazi tangu muda wa Tite wa miaka sita na nusu kumalizika baada ya Brazil kuondolewa na Croatia katika robo fainali ya Kombe la Dunia, Desemba mwaka jana.

Ederson alisema yeye na wachezaji wenzake wa Brazil wanamwona Ancelotti kama "kocha wa kipekee, kila mtu katika kundi lake anampenda ni mtu wa ushindi."

"Angalia tu CV yake. Tutajua baada ya muda mfupi kama atakuwa hapa au la," alisema Ederson.

"Natumai tunaweza kuwa na kocha mpya haraka. Ninahisi matarajio pia kwa sababu kuna uvumi mwingi. Je, ni Mbrazil au kocha wa kigeni? Pia tunaishi katika kipindi hiki kwa wasiwasi."

Kocha wa timu ya vijana chini ya umri wa miaka 20, Ramon Menezes, ndiye ataongoza mechi hiyo ya kirafiki Jumamosi.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,093,3

JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 23 NA 24 MACHI 2023
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/03/23 | 22:45 | Italy vs England | 2.76 | 3.25 | 2.63 |
| 02. 24/03/23 | 02:00 | La Equidad vs Chico | 2.52 | 2.90 | 2.80 |
| 03. 24/03/23 | 04:10 | America De Cali vs Junior Barranquilla | 2.21 | 3.14 | 3.35 |
| 04. 24/03/23 | 12:00 | Australia vs Ecuador | 2.69 | 3.17 | 2.69 |
| 05. 24/03/23 | 13:30 | Japan vs Uruguay | 2.85 | 3.23 | 2.50 |
| 06. 24/03/23 | 14:00 | South Korea vs Colombia | 3.02 | 3.13 | 2.44 |
| 07. 24/03/23 | 20:00 | Bulgaria vs Montenegro | 2.60 | 3.15 | 2.88 |
| 08. 24/03/23 | 20:00 | Denizlispor vs Boluspor | 2.77 | 3.23 | 2.28 |
| 09. 24.03/23 | 20:30 | Saint Brieuc vs Nancy | 2.68 | 2.95 | 2.68 |
| 10. 24/03/23 | 20:30 | Cholet vs FC Versailles 78 | 2.44 | 3.16 | 2.79 |
| 11. 24/03/23 | 20:30 | Paris 13 Atletico vs Bourg Peronnas | 2.67 | 2.98 | 2.67 |
| 12. 24/03/23 | 20:30 | Sedan vs Dunkerque | 2.43 | 3.11 | 2.85 |
| 13. 24/03/23 | 20:30 | Avranches vs Le Puy | 2.21 | 3.16 | 3.16 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MBAPPE NAHODHA MPYA UFARANSA




**PARIS,** Ufaransa

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe, ameteuliwa kuwa nahodha mpya wa Timu ya Taifa ya Ufaransa akirithi mikoba ya mlinda mlango wa Tottenham, Hugo Lloris, ambaye alistaafu soka la kimataifa Januari mwaka huu.

Mbappe mwenye umri wa miaka 24, ameichezea Ufaransa mara 66 tangu alipoichezea mechi yake ya kwanza mwaka 2017.

"Kylian anakidhi mahitaji yote ya kuwa na jukumu hili," alisema Kocha wa Ufaransa, Didier Deschamps, akikiambia Kituo cha Televisheni cha Ufaransa, TF1 katika mahojiano yatakayoonyeshwa Jumapili.

"Kwenye uwanja, katika maisha ya kikundi, yeye ni kiunganisha."

Shirikisho la Soka la Ufaransa (FFF), lilithibitisha kuwa Deschamps amemteua Mbappe kama nahodha na fowadi wa Atletico Madrid, Antoine Griezmann kuwa msaidizi wake.

Mbappe alikuwa mfungaji bora wa Kombe la Dunia mwaka jana alipoisaidia Ufaransa kufika fainali ya pili mfululizo ya Kombe la Dunia, ambapo walifungwa na Argentina kwa mikwaju ya penalti.

Alifunga mabao mawili kwenye fainali ya 2018 dhidi ya Croatia na alitajwa kuwa mchezaji bora chipukizi wa michuano hiyo huku Ufaransa wakitawazwa mabingwa wa dunia kwa mara ya pili.




## Arsenal yapata pigo kwa Tomiyasu

**LONDON,** England

MLINZI wa Arsenal, Takehiro Tomiyasu, atakosa msimu uliobaki baada ya kufanyiwa upasuaji wa jeraha la goti, klabu hiyo ya Ligi Ligi Kuu England, imetangaza.

Beki huyo wa kulia wa kimataifa wa Japan, Tomiyasu alitolewa nje dakika tisa kwenye mechi ya hatua ya 16-bora ya Ligi ya Europa wakati Arsenal ikiivaa Sporting CP ya Ureno baada ya kuteleza na kuumia goti.

Arteta alikuwa amesema wakati huo kwamba walikuwa na wasiwasi mara moja kwani mchezaji huyo wa kimataifa wa Japan mwenye umri wa miaka 24, "si mtu wa kutia chumvi mambo."

"Baada ya kubadilishwa kwake wakati wa mechi ya Alhamisi iliyopita ya Ligi ya Europa, tathmini zilizofuata zimethibitisha kwamba Takehiro Tomiyasu alipata jeraha kubwa kwenye goti lake la kulia," ilisema Arsenal katika taarifa yake.

"Tomi amefanyiwa up
suaji wa mafanikio jij
London Jumanne na atac
dolewa kwa muda uliosa
wa msimu huu."

Arsenal walitupwa n
ya Ligi ya Europa kwa m
waju ya penalti lakini ba
wako kileleni mwa Ligi K
wakiwa na tofauti ya poi
nane dhidi ya Manchest
City, ambao wana mche
mmoja mkononi.

Klabu hiyo ya Londo
kaskazini pia ilimpote
mlinzi William Saliba ku
kana na jeraha la mgon
katika mchezo huo huo.

## HABARI MICHEZO

# 395,265/-

# MILIONI 56/- ZA BONASI YA SUPA JACKPORT ZAENDA BAGAMOYO

**Na Mwandishi Wetu**

MFUGAJI kutoka Kata ya Migude wilayani Bagamoyo, Abibu Maulidi Omari, ameshinda Sh. 56,383,640, bonasi ya Supa Jackpot ya SportPesa baada ya kupatia kwa usahihi mechi 16 kati ya 17 za Supa Jackpot iliyochezwa mwishoni mwa wiki iliyopita.

**Akizungumza katika Ofisi za SportPesa, Dar es Salaam jana, Abibu, anasema alianza kucheza na SportPesa mwaka 2022, baada ya kukutana na mfanyakazi mwenzake ambaye alijiunga naye kazini katika Kampuni ya Ranch, iliyopo Bagamoyo, mwaka mmoja uliopita.**

"Mimi nilianza kucheza SportPesa mwaka jana, baada ya kukutana na Nurdin Kizenga, huyu jamaa alijiunga na kampuni yetu na kuajiriwa kama afisa mifugo, mwanzoni mwa mwaka jana. Kilichokuwa kinanishangaza, wote tuna simu janja, lakini yeye mara nyingi alipokuwa yuko huru alikuwa bize na simu yake.

"Mara kwa mara nilijiuliza ni nini kinamfanya awe bize na simu yake kila mara anapopata nafasi. Siku moja nilimuuliza ebana, mwenzangu mbona uko bize sana na simu yako. Bwana Nurdin alitabasamu na kuniambia yeye anabeti sana, kama njia nyingine ya kutafuta kipato cha ziada," Abibu alisimulia.

Aliendelea kwa kuelezea Nurdin anacheza na makampuni mengi ya kubeti, SportPesa ikiwa moja wapo lakini yeye ilibidi aanze kufuatilia kuhusu hayo makampuni kuhusu huduma na bidhaa zao.

"Nilijaribu kufuatilia kwa maana kampuni nyingi zipo mitandaoni na nikabaini SportPesa wanatangaza washindi wao karibu kila siku au kwa wiki hadi mara tatu. Nilipoendelea nikabaini washindi wengi ni wa Jackpot Bonus, na wanashinda vitita vikubwa vikubwa, kama milioni nne hadi 40 na ushehe.

"Viwango hivyo vya bonasi, pamoja na 'odds' kubwa za SportPesa zilinivutia mimi kubakia na SportPesa pekee. Niwe mkweli sijawahi kushinda kiasi chochote tangu nimeanza kucheza, ila nilikuwa nina imani ipo siku nitashinda hela nyingi."

Kuhusu mkeka wake wa Supa Jackpot Bonus, Abibu anasema yeye huwa na kawaida ya kufuatilia mechi za Jackpot kila zinapotoka na kwa wiki iliyopita mkeka ulipotoka yeye alikuwa barabarani peke yake anaendesha boda boda.

"Najua hamuwezi amini ni kwa namna gani niliweka huu mkeka ulionipa Supa Jackpot Bonus ya milioni 56 na ushehe. Ni hivi kwenye simu nilikuwa na kama 5,000 ambayo mara nyingi huwa naweka ili nisubiri kuweka mikeka ya Jackpot.

"Nilihamisha Sh. 3,000 kwenye akaunti ya SportPesa na kuweka mikeka mitatu ya Jackpot siku ya Alhamisi. Ilipofika Jumamosi. Mechi za Supa Jackpot zilianza kuchezwa. Wakati mechi zimeanza mimi na mshkaji wangu Nurdin ingawa hatukuwa pamoja tulikuwa tunawasiliana kwa simu kujuzana kinachoendelea kwenye mechi," alisema Abibu.

Aliendelea kusimulia kuwa Jumamosi mpaka mechi ya mwisho inachezwa ambapo Lazio ilikuwa inacheza alikuwa tayari ameshinda jumla ya mechi 7. Siku iliyofuata, yaani Jumapili kama kawaida yeye na Nurdin waliendelea kufuatilia matokeo mpaka tayari alikuwa amepatia mechi 15.

Kawaida Supa Jackpot ya mechi 17, ukipata mechi 15 unakuwa tayari umepata Jackpot, hivyo yeye alikuwa na furaha na kuingiwa na kiwewe zikiwa bado mechi mbili hazijachezwa.

"Unajua kaka muda ule ninajua nimepata timu 15, nilimpigia Nurdin na kumwambia -nimeshafikisha kiwango cha Supa Jackpot Bonus, na kichwa kilishaanza kuniuma kwa 'wenge' nililopata. Baadaye niliendelea kuangalia matokeo na mechi ya 16, ikawa imemalizika kuchezwa ambayo nayo nilipata.

"Hapo nilichanganyikiwa zaidi kwani nilikuwa nimebakiza mechi moja, ambayo ndio ilikuwa Rotherham VS Cardif. Mimi sikujua kama mechi ile imeahirishwa, kwa kuwa nilienda kulala kutuliza mizuka ambayo tayari ilikuwa imepanda.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano SportPesa, Sabrina Msuya alimpongeza mshindi huyo na kumtaka atumie ushindi wake kwa staha na awe balozi kwa mzuri kwa wengine.




Mshindi wa Jackpot Bonus, Abibu Omari, kutoka Bagamoyo akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 56 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 16 kati ya 17 kwenye Supa Jackpot ya SportPesa wiki iliyopita. **MPIGAPICHA WETU**

## Simba Queens, Yanga Princess zashikana tena

INATOKA UKURASA 24

kwenye nafasi ya nne ya msimamo wa ligi hiyo.

Kwenye Uwanja wa Chuo cha Mkwawa, Fountain Gate Princess ilikwea kileleni baada ya kuwatwanga vibonde wa ligi, Mkwawa Princess mabao 2-0, yote yakiwekwa wavuni na Neema Paul.

Bao la kwanza alifunga dakika ya 17 akiitendea haki pasi safi kutoka kwa Pivilidge Mupeti, na bao la pili alilifunga dakika ya 54 akiunganishwa kwa kichwa mpira wa kona uliopigwa na Nabbosa Ritticia.

## Rekodi Uganda vs Taifa Stars

INATOKA UKURASA 24

"Wachezaji wote tupo vizuri, tumejiandaa vizuri kwa mchezo dhidi ya Uganda, tunawaahidi Watanzania ushindi, ni kweli kuna wachezaji wapya wameitwa kwenye timu ya taifa na kocha ni mpya, Uganda tunawaheshimu wana timu nzuri wana wachezaji wazuri, lakini hayo yote hayawezi kuzuia sisi wachezaji kupambania taifa letu na timu yetu ya taifa, Taifa Stars. Mimi nasema katika hii michezo miwili ushindi Watanzania, watuombee dua tu," alisema Fei Toto."


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 25/03/23 | 18:00 | Doncaster Rovers vs Northampton Town | 2.50 | 3.15 | 2.70 |
| 02. 25/03/23 | 18:00 | Peterborough United vs Derby County | 2.55 | 3.30 | 2.50 |
| 03. 25/03/23 | 18:15 | Racing Santander vs Levante UD | 3.45 | 3.00 | 2.15 |
| 04. 25/03/23 | 18:15 | UD Ibiza vs Burgos CF | 2.33 | 2.80 | 3.30 |
| 05. 25/03/23 | 23:00 | Bogota FC vs Tigres FC | 2.27 | 2.85 | 2.90 |
| 06. 25/03/23 | 23:30 | Portland Timbers vs Los Angeles Galaxy | 2.14 | 3.30 | 2.70 |
| 07. 26/03/23 | 02:30 | DC United vs New England Revolution | 2.21 | 3.15 | 2.70 |
| 08. 26/03/23 | 02:30 | Charlotte FC vs New York Red Bulls | 2.39 | 3.00 | 2.60 |
| 09. 26/03/23 | 02:30 | Columbus Crew vs Atlanta United FC | 2.40 | 3.10 | 2.50 |
| 10. 26/03/23 | 03:30 | Houston Dynamo vs New York City FC | 2.44 | 3.10 | 2.45 |
| 11. 26/03/23 | 03:30 | Sporting Kansas City vs Seattle Sounders | 2.21 | 3.15 | 2.70 |
| 12. 26/03/23 | 04:05 | CF Correcaminos UAT vs CD Mineros de Zacatecas | 2.16 | 2.95 | 2.95 |
| 13. 26/03/23 | 06:05 | Pumas de Tabasco vs Raya2 Expansion | 2.49 | 2.95 | 2.49 |
| 14. 26/03/23 | 08:00 | Iwaki FC vs Machida Zelvia | 2.50 | 2.95 | 2.47 |
| 15. 26/03/23 | 15:30 | FC Dordrecht vs Helmond Sport | 2.47 | 3.15 | 2.39 |
| 16. 26/03/23 | 17:15 | SD Ponferradina vs CD Mirandes | 2.07 | 3.10 | 3.50 |
| 17. 26/03/23 | 17:15 | Real Zaragoza vs Albacete Balompie | 2.10 | 3.00 | 3.50 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 23/03/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3468 | Malaysia vs Turkmenistan | 1.83 | 3.55 | 4.31 |
| 14:00 | 3725 | Rio Ave U23 vs SC Farense U23 | 2.48 | 3.32 | 2.53 |
| 15:00 | 2987 | Hong Kong vs Singapore | 1.95 | 3.45 | 3.88 |
| 16:00 | 1275 | Madagascar vs Central African Republic | 1.81 | 3.41 | 4.47 |
| 16:00 | 3390 | Augsburg vs St. Gallen | 1.87 | 3.50 | 3.10 |
| 17:00 | 1397 | FK Zeleznicar Pancevo vs FK Radnicki Sremska Mitrovica | 1.54 | 3.24 | 6.58 |
| 17:00 | 3243 | FK Jedinstvo UB vs Sloboda | 2.07 | 3.04 | 3.35 |
| 17:00 | 3597 | FK Graficar Beograd vs OFK Vrsac | 1.75 | 3.38 | 4.10 |
| 17:00 | 4754 | FK Zlatibor vs Metalac | 2.77 | 2.93 | 2.45 |
| 17:00 | 5718 | FK Novi Sad vs Indjija | 2.05 | 2.98 | 3.50 |
| 18:00 | 1791 | America Mexico U20 vs Monterrey U20 | 1.55 | 3.65 | 4.60 |
| 18:00 | 3603 | Kazakhstan vs Slovenia | 4.01 | 3.31 | 2.01 |
| 19:00 | 2857 | Ghana vs Angola | 1.61 | 3.63 | 5.76 |
| 19:00 | 4400 | Zambia vs Lesotho | 1.30 | 4.80 | 10.67 |
| 19:00 | 4497 | Fenerbahce vs Zenit St Petersburg | 2.15 | 3.15 | 2.75 |
| 19:00 | 5135 | Congo vs South Sudan | 1.51 | 3.89 | 6.60 |
| 19:00 | 5585 | FK Babrungas Plunge vs Vmfd Zalgiris-3 | 2.13 | 3.43 | 2.87 |
| 20:00 | 1579 | Iran vs Russia | 2.27 | 3.17 | 3.28 |
| 20:00 | 3634 | Croatia U21 vs Israel U21 | 1.65 | 3.46 | 4.86 |
| 20:00 | 3684 | Hapoel Petach-Tikva W vs Hapoel Nir Ramat Hasharon W | 2.20 | 3.05 | 2.80 |
| 20:00 | 3793 | Maccabi Kishronot Hadera W vs Hapoel Beer Sheva W | 1.80 | 3.50 | 3.40 |
| 20:00 | 4607 | Maccabi Bnot Emek Hefer W vs MS Kiryat Gat W | 5.80 | 4.60 | 1.33 |
| 20:00 | 5518 | AS Tel Aviv University W vs Hapoel Katamon Jerusalem W | 3.85 | 3.70 | 1.64 |
| 21:00 | 5940 | Scotland U21 vs Sweden U21 | 2.84 | 3.31 | 2.24 |
| 21:30 | 5876 | Hungary vs Estonia | 1.50 | 4.14 | 6.67 |
| 21:45 | 1548 | Umm-Salal SC vs Al Arabi Doha SC | 4.77 | 3.79 | 1.60 |
| 21:45 | 2944 | Lekhwiya SC vs Al Sadd SC | 2.33 | 3.36 | 2.69 |
| 22:00 | 1260 | Gabon vs Sudan | 1.51 | 3.77 | 7.02 |
| 22:00 | 3454 | Saint-Martin vs Saint Kitts and Nevis | 6.64 | 4.56 | 1.37 |
| 22:00 | 4094 | Birmingham U21 vs Crewe U23 | 1.89 | 4.00 | 3.12 |
| 22:45 | 2190 | Bosnia and Herzegovina vs Iceland | 1.91 | 3.58 | 4.06 |
| 22:45 | 3435 | North Macedonia vs Malta | 1.40 | 4.67 | 8.25 |
| 22:45 | 3936 | Slovakia vs Luxembourg | 1.58 | 4.06 | 5.85 |
| 22:45 | 4179 | Denmark vs Finland | 1.38 | 4.57 | 9.35 |
| 22:45 | 4190 | Portugal vs Liechtenstein | 1.09 | 10.84 | 26.03 |
| 22:45 | 4320 | San Marino vs Northern Ireland | 32.66 | 7.84 | 1.12 |
| 22:45 | 5620 | Italy vs England | 2.82 | 3.20 | 2.61 |
| 23:00 | 4624 | CD La Equidad vs Atletico Huila W | 2.00 | 3.16 | 3.52 |

### IJUMAA - 24/03/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:00 | 5471 | Algeria vs Niger | 1.15 | 6.39 | 22.38 |
| 00:30 | 3407 | French Guiana vs Dominican Republic | 1.88 | 3.53 | 3.53 |
| 01:00 | 1744 | Brusque SC vs Concordia SC | 2.09 | 2.80 | 3.79 |
| 01:15 | 3693 | America De Cali SA W vs CA Bucaramanga Sa W | 1.06 | 6.80 | 19.00 |
| 02:00 | 1345 | Barbados vs Cuba | 5.80 | 4.04 | 1.47 |
| 02:00 | 1689 | Guadeloupe vs Antigua and Barbuda | 1.35 | 4.47 | 7.28 |
| 02:00 | 1792 | Cleveland SC vs Lionsbridge FC | 4.47 | 3.79 | 1.63 |
| 02:00 | 3991 | La Equidad vs Chico | 1.99 | 3.05 | 3.72 |
| 02:00 | 5283 | CF Atlante vs Tlaxcala FC | 1.31 | 4.58 | 8.33 |
| 02:30 | 4872 | Hartford City FC vs Lansdowne Bhoys FC | 1.76 | 3.52 | 4.04 |
| 02:30 | 5334 | Argentina vs Panama | 1.08 | 9.03 | 43.02 |
| 03:00 | 5557 | Suriname vs Mexico | 13.43 | 6.20 | 1.16 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Alhamisi Machi 23, 2023

Nipashe




Yanga yaivutia kasi Mazembe UKURASA 20



Straika wa Yanga, Mnigeria Chioma Wogu, akiwa katika nafasi nzuri ya kuumiliki mpira dhidi ya wachezaji wa Simba, Mwanahamisi Omari (katikati) na Vivian Corazone, kwenye mechi ya Ligi Kuu Wanawake iliyopigwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Simba Queens, Yanga Princess zashikana tena

**Na Adam Fungamwango**

KAMA ilivyokuwa mzunguko wa kwanza, timu za Simba Queens na Yanga Princess jana ziligawana tena pointi kwa kufungana bao 1-1 kwenye mechi ya raundi ya 12 ya Ligi Kuu Soka la Wanawake, iliyochezwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Desemba 23, mwaka jana timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1 kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza iliyochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Dar es Salaam.

Ni matokeo ambayo yameiengua Simba Queens kileleni, baada ya Fountain Gate Princess jana kuiadhibu Mkwawa Queens mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Chuo Kikuu cha Mkwawa, Iringa na kufikisha pointi 29, huku mabingwa hao watetezi wakishuka hadi nafasi ya pili wakiwa na pointi 27.

Tofauti na mechi ya kwanza ambayo Yanga Princess ilitangulia kupata bao, safari hii Simba Queens ilianza kupata bao la kwanza lililowekwa wavuni na Jentrix Shikangwa, akifunga kwa mguu wa kushoto na hii ni baada ya kupata pasi kutoka kwa Mkenya mwenzake Vivian Corazone.

Corazone ndiye aliyefunga bao la kusawazisha kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza, timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1, lakini safari hii ametoa 'assist.'

Straika raia wa Nigeria Chioma Wogu, ambaye aliifungia Yanga bao kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza, ndiye pia aliisawazishia Yanga Princess bao jana dakika ya 77.

Sare hiyo inaifanya Yanga Princess kufikisha pointi 22 ikiendelea kuwa

INAENDELEA UKURASA 23

# Rekodi Uganda vs Stars zashtua

## Samatta asema kocha amefanya yake kilichobaki ni wao, mabao yake na ya Okwi yatajwa...

**Dennis Fusi na Adam Fungamwango**

WAKATI kesho, Ijumaa Uganda na Tanzania zitamenyana kwenye Uwanja wa Suez Canal nchini Misri ambao haufungamani na upande wowote, katika mchezo wa kwanza wa kuwania kufuzu kwa michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika 2023, rekodi za miamba hiyo inapokutana, zinashtua zaidi.

**The Cranes ipo mkiani mwa Kundi F ikiwa na pointi moja pekee katika michezo miwili hadi sasa. Walichapwa mabao 2-0 na Algeria katika mechi yao ya ufunguzi na kutoka sare ya 1-1 na Niger katika mchezo uliofuata.**

Tanzania pia imejikusanyia pointi sawa na Uganda, baada ya kutoka sare ya bila kufungana na Niger na ikachapwa 2-0 na Algeria, hivyo itapania kufufua kampeni yao na imetaja wachezaji 30 kwa ajili ya mechi zao zijazo huku Uganda ikiwa na 'bunduki' zake 27.

### TAKWIMU

Hii itakuwa mechi ya 60 kwa mataifa hayo kukutana. Kati ya mechi 59 zilizopita, Uganda wameshinda mara 32, huku wakipoteza mara 12 tu na sare 15.

Katika mechi ya hivi karibuni, Tanzania na Uganda zilikutana Septemba 2022 katika mchezo wa kirafiki ambapo Taifa Stars ilishinda bao 1-0 na hivyo kuhitimisha mechi tatu mfululizo za kipigo.

Tanzania imeshinda michezo miwili pekee kati ya sita iliyopita, zote za ushindi zikiwa ni mechi za kirafiki (3-1 dhidi ya Jamhuri ya Afrika ya Kati na 1-0 dhidi ya Uganda).

Uganda wameshinda mchezo mmoja tu kati ya 13 iliyopita (1-0 dhidi ya Senegal katika michuano ya Mataifa ya Afrika 2022) na kupoteza mara sita.

Katika mchezo uliopita, winga Milton Karisa aliwaweka mbele kabla ya kipenga cha muda wa mapumziko, lakini Mahamadou Sabo akawasawazishia wageni katikati ya kipindi cha pili.

Kocha Mkuu wa The Cranes, Milutin Sredojevic 'Micho', katika kikosi chake pia amemjumuisha mfungaji wao mahiri katika historia, Emmanuel Okwi, aliyefunga mabao 28 kwa timu hiyo ya taifa. Pia kuna wachezaji wanne ambao hawajacheza kwenye kikosi hicho akiwamo fowadi wa Dundee United, Sadat Anaku.

Kwa Taifa Stars, itaendelea kumtegemea zaidi mshambuliaji wa KRC Genk, Mbwana Samatta, ambaye amefunga mabao 22 katika mechi 69 za timu ya taifa, akiwa nyuma ya Mrisho Ngassa mwenye mabao 25 katika historia ya timu hiyo ya taifa.

Akizungumzia mchezo huo, nahodha wa Taifa Stars, Samatta na kiungo Feisal Salum wamewaahidi mashabiki wa timu hiyo kuwa watafanya vema kwenye mechi ya kusaka nafasi ya kufuzu Afcon.

Samatta amesema wana imani kubwa ya kufanya vema chini ya kocha mpya, Adel Amrouche, ambaye amekuwa muwazi kwao, akiweka mbinu zake rahisi ili wachezaji wamwelewe.

"Kocha amejaribu kuwa wazi ili wachezaji wamwelewe, ni jukumu la wachezaji kumwelewa kile anachokitaka, akiweka mbinu na tukimwelewa basi tutapata kitu kizuri," alisema Samatta anayecheza soka la kulipwa KRC Genk ya Ubelgiji.

Akizungumzia wapinzani wao, nahodha huyo, alisema mechi itakuwa ngumu kwa sababu Uganda ni timu ngumu mno, hasa inapocheza dhidi ya Tanzania.

"Hakuna siku tunayocheza na Uganda mechi ikawa rahisi, siku zote ni mpinzani mgumu na huwa anatupa shida, tukubali huwa wanatupa shida Watanzania, ni wapinzani wagumu kucheza nao, na kwetu Watanzania mpinzani wetu mgumu zaidi Afrika Mashariki kucheza naye ni Uganda, lakini kadri siku zinavyozidi kwenda tunaanza kupunguza, itafikia hatua tutaweza kuwadhibiti kabisa, nakumbuka kuna mechi hivi karibuni tuliwafunga na hii tutahakikisha tunashinda," alisema Samatta.

Naye Fei Toto alisema kwa jinsi walivyojiandaa anaona mwanga kwa Stars kuweza kuibuka na ushindi nchini Misri.

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >